Tishio kwa Watetezi wa Haki za Binadamu linaweza kuelezewa kama “dhamira au dalili ya nia ya kudhuru, kuadhibu au kuumiza”. ‘Vitisho vinatumiwa sana ili kuwafanya watetezi wajione dhaifu, kuwa na wasiwasi, kumechanganyikiwa na kujihisi hawana msaada. Watetezi wa haki za binadamu wanapata vitisho kwa sababu ya athari ya kazi zao. Pia vitisho vingi vina lengo la kumfanya mtetezi aache kazi yake au kumlazimisha mtetezi atomize matakwa ya anayemtisha.

Vitisho huashiria uwezekano wa mtu mmoja kumdhuru mtu mwingine kimwili au kimaadili au kuharibu mali za mtu mwingine makusudi na kwa ghasia. Watetezi wanaweza kukabiliana na aina nyingi za vitisho katika mazingira ya migogoro, ikiwa ni pamoja vitisho vya kuwalenga watetezi, uhalifu wa kawaida dhidi ya watetezi na vitisho visivyo vya moja kwa moja.

Aina nyingi za vitisho zipo kama ifuatavyo;

- Ulengaji – Hivi ni vitisho vya mashambulio dhidi ya watetezi vinavyolenga kuzuia au kumlazimisha mtetezi au kikundi cha watetezi kuacha kazi yake ya utetezi au kuathiri tabia za watu wanaohusika na utetezi. Ulengaji kikawaida huhusiana sana na kazi zinazofanywa na watetezi husika, pamoja na maslahi na mahitaji ya watu wanaopinga kazi za watetezi.
- Tishio la mashambulizi ya kawaida ya jinai – Vitisho hivi hasa huhusiana na kazi za watetezi zinazowaweka katika maeneo hatarishi. Matukio mengi ya kulengwa yanafanyika kwa mtizamo wa kwamba ni “matukio ya kawaida” tu ya jinai.
- Vitisho visivyo vya moja kwa moja – Hutokea kutokana na madhara yanayosababishwa na mapigano ya kivita au ghasia, kama vile “kuwa sehemu ya hatari, wakati mbaya”. Hii hutokea hasa kwa watetezi wanaofanya kazi katika maeneo yenye vita.
- Vitisho vya matamko - kwa mfano kupokea tishio la kuuawa.

4.1 Vipengele vya Tishio

- Chanzo; Mfano mtu au kikundi cha watu ambao wameathirika na kazi ya mtetezi na kisha kutoa tishio.
- Lengo la tishio ambalo linahusishwa na athari za kazi ya mtetezi, na
- Njia iliyotumika; yaani jinsi tishio lilivyowasilishwa kwa mtetezi.

Vitisho ni mitego. Tunaweza kusema kwa kiasi fulani cha kejeri kuwa vitisho ni vya “kiikolojia”, kwa sababu vinalenga kufikia matokeo makubwa kwa uwekezaji wa nguvu kidogo. Mtu anayetoa kitisho amechagua kufanya hivyo, kuliko kuchukua hatua moja kwa moja - uwekezaji mkubwa wa nguvu. Lakini tujiulize, Kwa nini? Kunaweza kuwa na sababu kadhaa, na ni muhimu kuzitaja hapa:

- Mtu anayetoa vitisho ana uwezo wa kutekeleza vitisho lakini kwa kiasi fulani huogopa gharama za kisiasa zitazomkabili kwa kutekeleza vitisho waziwazi dhidi ya mtetezi wa haki za binadamu. Vivyo hivyo, vitisho vinavyotolewa na watu wasojulikana, vinaweza kutolewa kwa sababu hizohizo.
- Mtu anayetoa vitisho ana uwezo mdogo wa kuvitekeleza lakini anataka kufanikisha lengo lake kwa kuficha uwezo wake mdogo nyuma ya vitisho. Uwezo huu mdogo unaweza kuwa wa muda tu kutokana na vipaumbele vingine, au unaweza pia kudumu na kubaki mdogo. Lakini katika hali zote mbili, mambo yanaweza kubadilika muda wowote na kusababisha madhara ya moja kwa moja dhidi ya mtetezi baadaye.

4.2 Vitisho na Watetezi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania

Kama watetezi wengine wa haki za binadamu kwingineko duniani, watetezi nchini Tanzania pia wanakabiliwa na vitisho. Vitisho vinavyotokana na mamlaka husika zinazotishia kuyafutia usajili mashirika yasiyo ya kiserikali, vimejitokeza sana hasa kwa watetezi wanaofanya kazi za utetezi wa haki za wafugaji huko Wilayani Loliondo (NGONET na PINGOs Forum). Mnamo mwaka 2017, viliibuka vitisho vya kukifutia usajili Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) kilichoshutumiwa kujihusisha na harakati za kisiasa.

Katika hotuba ya Juni 22, 2017, Rais Magufuli alitoa katazo la utoaji wa huduma ya elimu bure kwa wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shuleni. Alidai kuwa hakubaliani na msimamo wa mashirika yasiyo ya kiserikali yanayolaani uvunjaji wa haki ya elimu kwa watoto.

Rais alisema kuwa “kwa muda ambao mimi nitakuwa rais, hakuna wanafunzi wajawazito wataruhusiwa kurudi shule”. Siku tatu baadaye, katika mkutano jijini Dodoma, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani Mhe. Mwigulu Nchemba pia aliyatishia mashirika ambayo yanapinga na kwenda kinyume na katazo hilo la Rais. Baadaye, Chama cha Wanawake Wanasheria (TAWLA) kilionywa kuhusu kuziongoza AZAKi zingine kwenye suala hilo la elimu kwa wasichana wanaopata ujauzito wakiwa shuleni.

4.3 Tathmini ya Vitisho

Mwisho wa siku, tunahitaji kujua kama tishio linaweza kutekelezwa au la. Ukiwa una hakika kwamba tishio hili haliwezekani kutekelezwa na mhusika, utakabiliana nalo tofauti kabisa na ikiwa una uhakika tishio husika linaweza kutekelezwa.

Malengo makuu mawili wakati wa kutathmini tishio ni:

Ili kupata habari nyingi iwezekanavyo kuhusu madhumuni na chanzo cha vitisho (vyote viwili vitakuwa vinahusishwa na athari za kazi zako za utetezi).

Ili kufikia maamuzi kama tishio litatekelezwa au la.

4.4 Hatua tano za kutathmini kitisho

Kubaini ukweli halisi juu ya tishio/vitisho. Ni muhimu kujua hasa kilichotokea. Hii inaweza kufanyika kupitia mahojiano au kwa kuuliza maswali kwa watu muhimu, na mara moja moja kupitia ripoti husika.

Kubaini kama kuna mfululizo wa vitisho vinavyohusiana katika kipindi husika. Ikiwa vitisho kadhaa vinatolewa mfululizo (kama ilivyo kawaida) ni muhimu kuangalia uhusiano wa kila kitisho, kama vile njia zinazotumiwa kutoa vitisho, nyakati ambazo vitisho vinaonekana, alama, taarifa zinazotolewa kwa maandishi au maneno, nk. Si rahisi kubaini uhusiano wa vitisho, lakini ni muhimu kwa kufanya tathmini sahihi ya vitisho hivyo.

Kubaini lengo la tishio. Kwa kawaida tishio huwa na lengo linalohusishwa na mlolongo wa athari za kazi za mtetezi kwa wahusika, unaoweza kubaini dhumuni au lengo la tishio husika.

Kumbaini anayetoa vitisho. (Hili linaweza kufanyika kwa kupitia hatua tatu za mwanzo kwanza). Jaribu kuchanganua kwa kina kadri iwezekanavyo. Kwa mfano, unaweza kusema kwamba “serikali” inakutisha. Lakini kwasababu serikali ni mjumuiko wa watendaji wengi, hivyo basi ni muhimu zaidi kujua ni sehemu gani ya serikali inaweza kuwa nyuma ya vitisho. Wafanyakazi kama vile “vikosi vya usalama” na “vikundi vya waasi” pia ni watendaji walio ndani ya mjumuiko huo. Kumbuka kwamba hata tishio lililosainiwa laweza kuwa la uwongo. Hii inaweza kuwa mbinu mbadala ya mtu anayetoa vitisho kwa siri kuepuka gharama za kisiasa na bado kufikia lengo lake la kuwatia hofu watetezi wa haki za binadamu na kujaribu kuwazuia kufanya kazi zao.

Fikia maamuzi ya busara kuhusu uhalisia wa utekelezwaji wa tishio kama linaweza kutekelezwa au la. Hatari ya tishio hutegemea mazingira husika. Huwezi kamwe kuwa na uhakika kabisa kuwa tishio litatekelezwa ama la. Kufanya utabiri kuhusu utekelezwaji wa tishio kutategemeana na hali ya hatari iliyopo itakayosababisha wahusika/mhusika kutekeleza tishio kwa mtetezi.

Sura ya

5

Matukio ya Kiusalama

5.0 Utangulizi

Tukio la kiusalama ni tukio lolote ambalo linaweza kuwaweka watetezi wa haki za binadamu (HRDs) au mashirika yao hatarini. Matukio ya kiusalama hutoa fundisho kwa watetezi na mashirika yao juu ya athari za kazi zao na jinsi maslahi ya watu mbalimbali yanavyoathirika. Pia huwapa fursa watetezi na mashirika yao kupitia upya mifumo na taratibu zao za ulinzi na usalama.

Mifano ya matukio ya usalama:

Wakati mwingine wapelelezi hutumwa kwenye ofisi za watetezi wa haki za binadamu ili kujua muda ambao watetezi huingia na kutoka ofisini, usafiri wanaotumia, rangi za gari zao, na kadhalika.

- Uvujaji wa taarifa juu ya kesi nyeti inaweza kusababisha vitisho vya kiusalama kama vile kukamatwa na kuwekwa kizuizini, kufwatiliwa na kutishiwa na mtu anayehusika katika ukiukwaji wa haki za binadamu.
- Ikiwa wageni hawakaguliwi vizuri na vitambulisho vyao havirekodiwi, mtu yeyote anaweza kuingia katika ofisi za watetezi na kufanya uhalifu au kuathiri usalama wao. Kukosekana kwa ushahidi wa ugeni dhidi ya wahusika, kisheria kunaweza kusababisha wasiadhibiwe.

'Tukio la kiusalama ni "kiashiria cha kidogo sana" katika kupima hali ya usalama na pia huashiria upinzani/shinikizo juu ya kazi yako kama Mtetezi wa Haki za Binadamu. Usiache matukio ya kiusalama yapite bila kutambuliwa!'

5.1 Hali ya watetezi wa haki za binadamu (HRDs) nchini Tanzania

Kama itakavyoelezwa hapa chini, kuyatambua matukio ya kiusalama kunahitaji ufahamu juu ya dhana ya ulinzi na usalama kwa watetezi wa haki za binadamu. Kwa kawaida, watetezi wengi wa haki za binadamu ambao hawazifahamu kanuni za ulinzi na usalama huyachukulia matukio ya kiusalama kimzaha na hawawezi kuyachambua.

Tanzania kwa mfano, wakati wa kuanzishwa kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), watetezi wachache sana walikuwa na ujuzi wa masuala ya ulinzi na usalama. Kulingana na tafiti THRDC ya mawaka 2013 juu ya tathmini ya mahitaji ya watetezi nchini, watetezi 135 tu kati ya 2000 kutoka mashirika ya haki za binadamu na vyombo vya habari walikuwa wameshawahi kuhudhuria mafunzo ya usalama kwa watetezi, aidha nchini au nje ya Tanzania.

Kuanzishwa kwa THRDC hususani dawati lake la ujengaji uwezo na uwezeshaji, umefumbua macho ya watetezi wengi kupitia mafunzo ya usalama na wameweza kutambua asili ya mazingira yao ya kazi, hivyo ni rahisi kwao kuyatambua na kuyakabili matukio ya kiusalama dhidi yao.

Kwa mfano haya hapa ni baadhi ya matukio yaliyoripotiwa ya usalama yaliyotajwa na watetezi waliopata mafunzo;

- Ndugu Deus Kibamba (Mkurugenzi Mtendaji wa zamani, Jukwaa la Katiba)

  Mnamo tarehe 12 Aprili 2013, kati ya saa 5 asubuhi hadi saa 6 mchana, gari aina ya Land Cruiser lenye rangi ya bluu, lenye na namba za usajili T126 CCG, lilionekana likiwa limepaki kwenye eneo la ofisi za Jukwaa la Katiba, likiwa na watu sita ndani, ambapo wawili kati yao walielekea geti kuu la ofisi hiyo kumuulizia Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Ndugu Deus Kibamba pamoja na Mratibu wake Bi. Diana Kidala. Wawili hawa walijifanya kuwa na undugu na Bwana Kibamba. Cha kushangaza, waliomba pia namba zake za simu baada ya kutambua kwamba wamegonga mwamba. Baadae, wawili hawa walionekana wakijadiliana nje ya ofisi za Jukwaa la Katiba kwa muda wa takribani lisaa limoja. Jukwaa la Katiba iliripoti tukio hilo la kiusalama kwa Jeshi la Polisi na wakati huohuo THRDC ilitoa tamko kwa vyombo vya habari kulaani tukio hilo na kuchukua hatua za kulifanyia tukio hilo uchunguzi.

- Ndugu Antony Lyamuda, Mkurugenzi Mtendaji wa Civil Education is the Solution to Poverty and Environmental Management (CESOPE)

  Mnamo mwezi Machi 2013, Bw. Lyamunda alipokea vitisho na kufwatiliwa mara kwa mara na watu wasiojulikana. Katika jitihada za kuyakabili matukio haya ya kiusalama, Bw. Lyamunda alisaidiwa kwa kuondolewa nje ya nchi kwa muda.

- Ndugu Maxence Melo, Mkurugenzi Mtendaji wa Jamii Media (JamiiForums); kama moja wapo ya tovuti zinazotumiwa na watumiaji mitandaoni kuandika, kujadili na kufuatilia masuala mbalimbali ya muhimu katika jamii. Aliripoti vitisho na matukio kadhaa ya kiusalama dhidi yake kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), ambapo matukio haya yalijumuisha zaidi ya barua tano alizoandikiwa na jeshi la polisi mnamo mwaka 2016, akitakiwa kufichua anwani za IP za baadhi ya watumiaji wa JamiiForums. Jeshi la polisi lilimshtaki kupitia kifungu namba 32 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015.

- Ndugu Onesmo Olengurumwa, Mratibu Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)

  Kati ya mwaka 2017 na mwaka 2018, Bw. Onesmo Olengurumwa alihojiwa mara kadhaa kuhusu utaifa wake kutokana na kazi yake ya utetezi wa haki za binadamu. Alikamatwa na kushtakiwa mwaka 2017 wakati wa uzinduzi wa kitabu cha mtetezi kijana Alphonce Lusako. Watu wasiojulikana walionekana maeneo ya nyumbani kwake wakati yeye hayupo wakiwauliza watoto wake kuhusu mahali alipo baba yao.

5.2 Jinsi ya Kukabiliana na Matukio ya Kiusalama

Athari za kazi za watetezi wa haki za binadamu, mara nyingi zinaweza kupimwa kupitia mtazamo wa jamii yao. Wakati tukio la kiusalama linapotokea, mtetezi anapaswa kuchukua hatua kadhaa ili kuhakikisha kwamba tukio hilo linashughulikiwa vizuri. Hatua hizi zinaweza kutofautiana kwa matukio tofauti.

Hatua ya 1: Kuripoti Tukio

Mtetezi wa Haki za Binadamu anapopata tukio la kiusalama, anapaswa kuripoti au kutoa taarifa ya tukio husika kwa mtu maalumu anayesimamia masuala ya usalama katika shirika lake au kwa mkurugenzi wa shirika lake. Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) pia wanaweza kuripoti moja kwa moja kwa Afisa Ulinzi na Usalama wa THRDC katika makao makuu ya THRDC.

Taarifa muhimu katika ripoti hii inapaswa kujumuisha:

- Ni nani anayeripoti?
- Nini kimetokea? Kilitokea wapi? Kilitokea lini? (toa maelezo sahihi na ya kina kadri iwezekanavyo);
- Ni nani aliyehusika, na maelezo gani yametolewa na waathirika wa tukio hilo?;
- Nini athari ni juu ya wale walioathirika, na maelezo ya hali yao ya sasa;
- Ni nani aliyefanya tukio hilo, elezea kwa ufupi idadi, aina ya silaha, msaada wa awali uliotolewa, matukio ya baada ya tukio la kiusalama;
- Muhtasari wa hali ya muda huo na ikiwa bado kuna matatizo au la;
- Ikiwa ndio, ni maamuzi gani na hatua gani zimechukuliwa/zimependekezwa na aliyeripoti katika kukabili tukio la kiusalama.

Kumbuka: Ripoti ya tukio la kiusalama inaweza kuwa katika maandishi au maneno. Hata hivyo, tukio hilo linapaswa kuwekwa katika maandishi ili kuzuia kupoteza ukweli.

Hatua ya 2: Kuchunguza Ukweli

Wakati wa kuchunguza ukweli, masuala kadhaa yanahitaji kuzingatiwa: Ni nani atakuwa kahusika?, Ni wapi tukio la kiusalama lilitokea?, Kuna yeyote aliyejeruhiwa au mali iliyoharibiwa?, Ni nini lengo la wahusika?. Haya masuala yataamua hatua za kuchukua katika kukabiliana na tukio la kiusalama. Kufikia hapo, unapaswa kujua uzito wa tukio husika ili kujua kama tukio hilo ni dogo au kubwa.

Hatua ya 3: Kukabili au Kutokabili Tukio la Kiusalama

Uchunguzi unapoonesha kuwa tukio la kiusalama ni kubwa, watetezi wa haki za binadamu wanapaswa kuchukua hatua stahiki. Hatua ya kuchukua hutegemeana na hali ya tukio husika la kiusalama. Ikitokea ofisi imevamiwa, vitasa vipya na mifumo ya usalama inapaswa kuwekwa. Ikiwa tukio la kiusalama litachukuliwa kuwa la kawaida, watetezi wanaweza wasichukue hatua kubwa lakini wanapaswa kulirekodi tukio hilo kwa ajili ya marejeo baadaye.

Sura ya

6

Kuzuia na Kukabiliana na Mashambulizi

6.1 Utangulizi

Kushambulia ni mchakato, pia ni kitendo. Unapofanya uchambuzi vizuri wa mashambulizi mara nyingi utagundua kwamba shambulio ni hitimisho la migogoro, vitisho na makosa ambayo yamekuwepo tangu muda mrefu.

Mashambulizi dhidi ya Watetezi wa Haki za Binadamu ni matokeo ya angalau sababu tatu zinazoshabihiana:

- Mshambuliaji binafsi. Mashambulizi dhidi ya Watetezi wa Haki za Binadamu mara nyingi ni matokeo ya michakato ya kimawazo na tabia ambazo tunaweza kuzielewa na kujifunza kutokana na mawazo au tabia hizo hata kama ni kinyume cha sheria. Muhusika atahitaji kuwekeza katika njia za kukusanya taarifa (matukio ya kiusalama) kuhusu Mtetezi wa Haki za Binadamu aliyelengwa.
- Misingi na vichocheo vinavyopelekea mshambuliaji kuona shambulizi kama chaguo. Watu wengi ambao wanawashambulia Watetezi wa Haki za Binadamu huona kushambulia kama njia ya kufikia lengo au 'kutatua tatizo'.
- Mazingira yanayopelekea mashambulizi kufanyika.

6.2 Hali kwa ufupi juu ya mashambulio kwa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania.

Tofauti na miaka iliyopita, Tanzania hivi karibuni imeshuhudia kuongezeka kwa mashambulizi, upotevu na utekaji nyara wa Watetezi wa Haki za Binadamu na waandishi wa habari unatekelezwa na watu wasiojulikana. Kuzuia kwa mikutano ya ndani wa Watetezi wa Haki za Binadamu na kukamatwa kiholela kumeenea.

Katika miaka mitano ambayo Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania umekuwa ukifanya kazi, waandishi wa habari, maafisa wa polisi na Watetezi wa Haki za Binadamu wengine wamekuwa waathirika wakubwa wa mashambulizi. Mwaka 2017 kwa mfano, ofisi tatu za wanasheria (makampuni ya wanasheria) zilivamiwa na moja kati ya hizi ni (Kampuni ya Mawakili ya IMMMA) iliyopigwa bomu na kusababisha hasara kubwa ya mali na hofu ndani ya taaluma ya sheria. Mnamo Septemba 2017 kulikuwa na mashambulizi ya mabaya kwa Mtetezi wa Haki za Binadamu na Rais wa Chama Cha Mawakili Tanganyika, Mheshimiwa. Tundu Lissu. Washambuliaji

wa Watetezi wa Haki za Binadamu tajwa hapo juu hawajawahi kutambuliwa, hawajakamatwa na kufikishwa mahakamani ili kukabiliana na mashtaka yanayowapasa.

6.3 Nani ni hatari kwa Watetezi wa Haki za Binadamu?

Kwa ujumla, ni yeyote anayefikiri kuwa kushambulia Mtetezi wa Haki za Binadamu ni njia sahihi au ya muhimu ili kufikia lengo.

6.4 Ufuatiliaji na namna ya Kukabiliana nao

Mashambulizi mengine yanatanguliwa na vitisho. Mengine sio. Hata hivyo, tabia ya watu wanaopanga mashambulizi ya vurugu mara nyingi huonyesha ishara za hila, kwa sababu wanahitaji kukusanya taarifa kuhusu wakati sahihi wa unyanyasaji, kupanga jinsi ya kufikia lengo lao, na jinsi ya kukwepa.

Ufuatiliaji wa Watetezi wa Haki za Binadamu hufanyika kwa kawaida mahali pa kazi, nyumbani au mahali ambapo wanependelea kuonekana. Mashambulizi hufanyika wakati wa hatari zaidi au wakati wa uwezo dhaifu wa Watetezi wa Haki za Binadamu. Mtu yeyote katika eneo lako, kama vile walinzi au wabeba mizigo katika majengo, wafanyabiashara wanaotembeza bidhaa karibu na mlango wa kuingia, watu katika magari ya karibu, wageni, nk, ni rahisi kuangalia mienendo yako.

Ufuatiliaji unaweza kutumika kwa madhumuni kadhaa

- Kufahamu shughuli gani zinazofanyika, wakati gani na pamoja na nani.
- Kutumia taarifa hizi baadaye ili kushambulia watu binafsi au mashirika.
- Kukusanya taarifa muhimu ili kutekeleza mashambulizi.
- Kukusanya taarifa kwa hatua za kisheria au unyanyasaji mwingine (bila madhara ya moja kwa moja).
- Kukutisha wewe, wafuasi wako au watu wengine wanaofanya kazi na wewe.

Kwa hiyo ni muhimu kuchunguza na kuchambua ishara yoyote inayoonyesha uwezekano wa mashambulizi (kukabiliana na ufuatiliaji). Hii inajumuisha:

- Kuchunguza kwa kiasi kikubwa wale ambao wanaweza wakawa wanakufwatilia
- Kutambua mienendo ya watu wa eneo lako na mabadiliko katika mtazamo wao
- Kumshirikisha mtu wa tatu unayemwamini kuwaangalia kwa niaba yako bila kuwafwata moja kwa moja au bila wao kujua
- Kabla ya kufika nyumbani unaweza kumuuliza mwanafamilia au jirani anayeaminika kuangalia kwa ukaribu na (kwa mfano. kubadilisha tairi la gari), ili uone kama kuna mtu anasubiri ufike.
- Kutambua na kuchambua matukio ya usalama
- Kutambua uwezekano wa tishio unaoweza kufanywa

Ni muhimu kutambua kwamba;

- Kushambulia mtetezi si rahisi na inahitaji rasilimali.

  Ufuatiliaji unahitajika ili kutambua harakati za mtu binafsi na eneo bora la kushambulia. Kufikia lengo na kutengeneza ufanisi, wa haraka pia ni muhimu. (Hata hivyo, kama mazingira yanafaa sana kwa mshambuliaji, mashambulizi ni rahisi kufanyika.)

- Watu ambao wanashambulia watetezi kawaida huonyesha kiwango cha uthabiti.

  Mashambulizi mengi yanalenga watetezi ambao wanahusika sana katika masuala yanayoathiri mashambulizi. Kwa maneno mengine, unyanyasaji haufanyiki ovyo ovyo au bila kusudi, bali hukidhi maslahi ya washambuliaji.

- Sababu za kijiografia

  Kwa mfano, mashambulizi dhidi ya watetezi katika maeneo ya vijijini yanaweza kuwa hayaufikii umma kwa kiasi kikubwa na hivyo kusababisha udhibiti mdogo wa watekelezaji wa sheria na ngazi ya kisiasa kuliko mashambulizi katika maeneo ya mijini. Mashambulizi dhidi ya makao makuu ya shirika au mashirika ya yenye sifa kubwa katika maeneo ya mijini huwa yanadhibitiwa zaidi.

- Chaguo na maamuzi hufanywa kabla ya kushambuliwa.

  Watu wanaopanga shambulio dhidi ya shirika la watetezi wanapaswa kuamua aidha kuwashambulia viongozi au wanachama wa ngazi ya chini, na kuchagua moja kati ya hao (dhidi ya muhusika mkuuna hivyo kupelekea kutumika kwa gharama kubwa kwa washambuliaji) au mfululizo wa mashambulizi (yanayoathiri uanachama wa shirika). Uchunguzi mdogo uliofanyika juu ya mashambulizi dhidi ya watetezi unaonyesha kwamba mikakati yote iliyotajwa hapo juu mara nyingi hutumika.

Sura ya

7

Kukamatwa, kuwekwa Kizuizini na Kushitakiwa kwa Mtetezi wa Haki za Binadamu

7.0 Utangulizi

Ni muhimu kutambua kwamba, kukamatwa, kuwekwa kizuizini na kushitakiwa kwa mtetezi au mtu mwingine yeyote kunaongozwa na sheria tofauti na vyombo tofauti vya utekelezaji wa sheria. Kwahiyo, Mtetezi wa Haki za Binadamu anahitaji kuwa na ufahamu mpana au kwa kifupi kuhusu haki zake wakati matukio yoyote yaliyotajwa hapo juu yanapotokea.

7.1 Hali ya kukamatwa, kuwekwa kizuizini na kushitakiwa kwa mtetezi

Hali ya kukamatwa, kuwekwa kizuizini na kushitakiwa kwa Watetezi wa Haki za Binadamu nchini Tanzania imeongezeka katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Hali hii imesababishwa ya matumizi mabaya ya nguvu, kutokujali, hali ya kisiasa, kutokuheshimu utawala wa sheria na utawala bora. Watetezi wa Haki za Binadamu wamekuwa kundi lililoathirika zaidi katika matukio haya. Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania chini ya Dawati lake la Ulinzi la mwaka 2016 na 2017 liliweza kurekodi matukio zaidi ya 70 ya ukiukwaji wa haki za binadamu ikiwa ni pamoja na kukamatwa kiholela, kuwekwa kizuizini kinyume cha sheria, na mashtaka ya kughushi. Matukio haya sio tu kwamba yanakiuka haki ambazo watetezi wa haki za binadamu wamepewa lakini pia hufanya mazingira yao ya kazi kuwa mabaya zaidi.

7.1.1 Kukamatwa

Kitendo cha kumkamata mtu kimehusishwa na aina mbalimbali zakanuni za kiutendaji. Kuna wakati ambapo polisi hutumia nguvu nyingi wakati wa kukamata, hata pale ambapo mtuhumiwa anakuwa yupo tayari kwenda kwenye kituo cha polisi bila shuruti. Inaonekana kwamba polisi polisi wamejijengea tabia kwamba hatua ya kwanza katika kushughulika na mtuhumiwa ni kumdharau na kumdhalilisha mbele ya ndugu, jamaa na marafiki zake. Sheria haijaelekeza polisi kufanya kazi katika mazingira hayo.

Hatua ya kwanza ambayo sheria inaelekeza ni kukamatwa kwa mtuhumiwa tu. Mara nyingi pale ambapo mtu, anaambiwa kwamba yupo chini ya ulinzi, anapaswa kukamatwa na kuambiwa sababu za kukamatwa kwake. Ni pale tu ambapo mtuhumiwa hukataa kutii agizo la kukamatwa

ndipo polisi anaruhusiwa kugusa mwili wa mtu au kumfunga pingu. Ikiwa mtuhumiwa atakataa kukamatwa, basi polisi wanaruhusiwa kutumia nguvu ya kawaida kuweza kumkamata mtuhumiwa. Muhimu kujua kwamba mtuhumiwa ana haki ya kufahamishwa kosa ambalo anatuhumiwa kabla ya kukamatwa na polisi.

Wakati polisi wanapomkamata mtu, huondoa haki ya msingi ya mtu huyo kuwa huru. Kwa hiyo, kuna taratibu kadhaa ambazo polisi lazima wazifuate kabla ya kumkamata mtu kisheria ili kuhakikisha haki za binadamu zinazingatiwa.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ya mwaka 1985, mtu aliyekamatwa ana haki kadhaa za kuzingatiwa. Hivyo, afisa anayemkamata mtuhumiwa anapaswa kuhakikisha kwamba lazima azingatie taratibu zote za kisheria za kumkamata mtuhumiwa.

(a) Ni wakati gani afisa anaweza kumkamata mtu?

Kuna idadi ndogo tu ya mazingira ambayo afisa anaweza kumkamata mtu.

- Afisa mwenyewe aliposhuhudia kitendo cha uhalifu;
- Afisa ana sababu ya kuamini kuwa mtu huyo aliyekamatwa alifanya uhalifu;
- Afisa ana hati ya kukamata iliyotolewa na hakimu.

(b) Utaratibu wa kukamata Mtuhumiwa

Utaratibu juu ya kile ambacho afisa anapaswa kufanya wakati wa kukamata nchini Tanzania umetolewa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, ya mwaka 1985. Kwa ujumla, kukamatwa hutokea wakati mtu anayekamatwa anaamini kuwa hayuko huru kuondoka. Afisa hahitaji kumfunga pingu mtuhumiwa, au kumuweka mtuhumiwa katika gari la polisi ingawa polisi mara nyingi hutumia mbinu hizi kujikinga. Polisi pia wanapaswa kusoma Sheria ya Mwenendo wa Makossa ya Jinai, 1985 wakati wa kukamata.

Hata hivyo, polisi lazima asome mbele ya mtuhumiwa haki zake chini ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 1985 kabla ya mahojiano, kama ambavyo idara nyingi za polisi husisitiza kwamba Haki za watuhumiwa zisomwe kabla ya kukamata. Kwa njia hii, polisi wanaweza kuanza kumhoji mtuhumiwa mara moja, na pia, taarifa yoyote inayotolewa na mtuhumiwa inaweza kutumika dhidi yao. Hatimaye, ingawa polisi daima humwambia mtuhumiwa kwanini amekamatwa, wanaweza kutokuwa na wajibu wa lazima wa kisheria kufanya hivyo.

Moja ya kanuni inayotumia duniani kote ambayo maafisa wa polisi wote wanapaswa kufuata ni kwamba hawaruhusiwi kutumia nguvu nyingi au kumuadhibu mtuhumiwa kikatili. Hii pia imewekwakwa wazi chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi ya mwaka 1969. Kwa ujumla, maafisa wa polisi wanaruhusiwa kutumia kiasi cha chini cha nguvu zinazohitajika ili kujilinda na kumuweka mtuhumiwa chini ya ulinzi wa polisi. Ndiyo sababu watu wanashauriwa kamwe kutokupinga kukamatwa au kujibizana na polisi. Kadri mtuhumiwa anavyopambana kukataa kukamatwa, nguvu zaidi inahitajika kwa polisi kufanya kazi yao. Ikiwa mtuhumiwa anadhani kukamatwa kwake sio halali kisheria au si sahihi anaweza kupinga kukamatwa kwake baadae kwa msaada wa mwanasheria, na ikiwa ni kweli, anaweza kufungua kesi ya haki ya madai.

(c) Upekuzi

Upekuzi inabidi ufanye kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa, kwakuwa huingilia faragha na uhuru wa mtu kwa mujibu wa na Katiba. Hivyo ni muhimu kupata kibali cha upekuzi kutoka kwa mamlaka husika kabla ya kumkamata mtuhumiwa.

Zipo aina mbili za upekuzi;

- Kwanza ni kibali kutoka katika kituo cha polisi husika. Kibali hiki kinaweza kutolewa kwa mtu yeyote ikiwa ni pamoja na maafisa wa polisi.
- Kibali chaa pili ni kibali cha upekuzi kinachotolewa na mahakama.

7.1.2 Kuwekwa kizuizini

Ikumbukwe kwamba, kuwekwa kizuizini kwa Mtetezi wa Haki za Binadamu au mtu mwingine yeyote kunazuia uhuru wa mtu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndiyo maana kuwekwa kizuizini kwa mtu kuna kikomo cha muda. Kikomo kikubwa cha muda uliopo kisheria ni masaa 24 ambayo mtu aliyekamatwa anatakiwa kupelekwa mahakamani au kupewa dhamana ya polisi.

Endapo Mtetezi wa Haki za Binadamu au mtu mwingine yeyote atakaa chini ya ulinzi wa polisi au sehemu nyingine kizuizini bila ya kupelekwa mahakamani au kupewa dhamana ya polisi, inashauriwa kwamba maombi ya dhamana na / au maombi ya mtuhumiwa kuletwa mahakamani yanapaswa kupelekwa mahakamani ili kuomba amri ya mahakama kwamba mtu huyo aletwe mahakamani ili kukabiliana na mashtaka yanayomkabili. Katika kupeleka maombi haya, Mtetezi wa Haki za Binadamu anahitaji kupata msaada wa mwanasheria ambapo pia Mtanadao wa Watetezi wa Haki za Binadamu unaweza kuingilia kati na kusaidia.

7.1.3 Mashtaka

Ni muhimu kutambua kwamba, moja ya huduma za ulinzi zinazotolewa na Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu ni uwakilishi wa mahakamani. Kwa hiyo Watetezi wa Haki za Binadamu wanaokumbana na changamoto za kisheria wanapaswa kutoa taarifa kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu kwa msaada zaidi. Hata hivyo, tunasisitiza Mtetezi wa Haki za Binadamu kuelewa mambo kadhaa yanayohusiana na mashtaka kama mkakati binafsi wa kujilinda. Katika sehemu hii Mtetezi wa Haki za Binadamu atadhaniwa kuwa ni mtuhumiwa. Uendendeshaji wa mashitaka kwa kawaida hufanyika kulingana na hatua zifuatazo;

(a) Hati ya mashtaka (mashtaka)

Shitaka ni msingi wa kufungua kesi ya jinai dhidi ya mtuhumiwa. Hii ni hati ambayo inaelezea makosa na vifungu vya sheria ambavyo mtuhumiwa amevunja, pamoja na taarifa zake binafsi. Mwendesha Mashtaka ataandaa mashitaka ikiwa kesi hiyo inasikilizwa na mahakama ndogo au taarifa kama makosa yanaweza kusikilizwa tu na Mahakama Kuu. Haya ni makosa ambayo yanasikilizwa na Mahakama Kuu tu kama vile ndugu wa damu kuwa katika mahusiano ya kimapenzi, mauaji, uchomaji na uasi.

(b) Kukiri au kukataa mashtaka

Hapa mshitakiwa anatakiwa kukiri au kukataa mashtaka aliyosomewa. Mshitakiwa atatakiwa na mahakama kukubali au kukataa mashtaka dhidi yake. Ikiwa mshitakiwa atakiri kuwa ana hatia lazima kukiri kwake kusiwe na utata, pakiwa na utata tu mahakama itasema mshitakiwa hajakiri kuwa ana hatia. Ikiwa mahakama itathibitisha kuwa mtuhumiwa ana hatia, mwendesha mashtaka ataruhusiwa kuendelea na kesi yake. Ikiwa imeahirishwa mshitakiwa atakuwa na nafasi ya kuomba dhamana, ikiwa kosa lake lina dhamana. Ikiwa mshitakiwa amekiri kuwa ana hatia basi utaratibu utarukwa hadi kumuachia huru au kuhukumiwa.

(c) Dhamana ya Mahakama

Mara nyingi ikiwa mtuhumiwa amekiri kuwa na hatia, maombi ya dhamana hayatumiki tena na dhamana haiwezi kutolewa. Baada ya kukiri au kukataa kosa mtu anapelekwa rumande au anaachiwa kwa dhamana. Dhamana ni haki ya kikatiba chini ya Ibara ya13 (6) (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, ambapo mtu hudhaniwa kuwa hana hatia hadi mahakama itakapothibitisha kwamba mtu huyo ni mkosaji. Kuna makosa yasiyo na dhamana kama vile Uhaini, wizi wa kutumia silaha, unajisi na mauaji chini ya kifungu cha 148 (5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai. Dhamana ya polisi inaweza kutolewa kabla ya kesi kwenda mahakamani; dhamana ya mahakama hutolewa wakati ambao kesi imeshapelekwa mahakamani.

(d) Usikilizaji wa Awali

Hii ni hatua muhimu ambapo pande zote zinakutana na rasimu kuhusu uhalisia wa maswala wanayokubaliana ili kuharakisha usikilizwaji wa kesi. Pande zote zinapaswa kukutana na kuamua juu ya mambo ambayo hayana mgogoro na mambo haya hayatakiwi kuletwa wakati kesi inaendelea na kila pande haitakiwi kuthibitisha chochote kuhusu masuala hayo kasoro yale mambo tu ambayo yapo kwenye mgogoro.

(e) Hatua ya Usikilizwaji wa Kesi

Huu ndio wakati kesi inapangwa kwa ajili ya kusikilizwa au kutajwa na mwendesha mashtaka anapaswa kuthibitisha mbele ya mahakama kama kuna kesi dhidi ya mshitakiwa au sio laa.

Kesi upande wa Mwendesha Mashtaka

Hii ni hatua ambapo mwendesha mashtaka anapaswa kuwasilisha kesi yake, ambapo mwendesha mashtaka atawaita mashahidi kutoa ushahidi wao na kuwasilisha ushahidi wowote mwingine unaounga mkono kesi yao, kwa ajili ya mahakama kuamua kama kuna kesi ya kujibu au laa. Ni katika hatua hii ambapo shahidi atahojiwa kwa mara ya kwanza kisha kuhojiwa na upande wa utetezi hatimaye kufuatiwa tena na uchunguzi wa upande wa mashtaka. Muhimu; kwa ujumla, wajibu wa kuthibitisha mashtaka upo upande wa mwendesha mashtaka na kiwango cha kuthibitisha ni bila kuacha shaka ya aina yoyote.

(f) Kuwa au kutokuwa na kesi ya kujibu.

Hii ndio hatua ambapo mahakama inapaswa kuamua kama kuna kesi ya kujibu au laa, kwa kuzingatia ushahidi uliotolewa na upande wa mwendesha mashtaka. Ikiwa hakuna kesi ya kujibu mahakama itamuachia huru mshtakiwa, ikiwa kuna kesi ya kujibu mshtakiwa atakuwa na nafasi ya kutoa ushahidi wake.

(g) Kesi ya Upande wa Utetezi

Kimsingi hapa timu ya upande wa utetezi itawasilisha ushahidi wake, shahidi ataongozwa na wakili wa utetezi, pia na upande wa mashitaka na mwisho ataongozwa tena na upande wa utetezi.

(h) Uwasilishaji wa mwisho.

Huu ni muhtasari wa uwasilishaji kamili kutoka kila upande; upande wa utetezi utakuwa wa kwanza kufanya uwasilisho wao wa mwisho kisha kufuatiwa na upande wa mashtaka. Uwasilishaji wa mwisho unaweza kuwa wa mdomo au wa maandishi, hii lazima iwe na ruhusa ya mahakama.

(h) Kumuachia huru au kumpa kifungo mshitakiwa

Hii ni hatua ambapo mahakama itaamua kwa kutegemea uwasilishaji wa mwendesha mashitaka na upande wa utetezi kama mshitakiwa anapatikana na hatia au la. Kwa hivyo mshitakiwa anaweza kupatikana kuwa hana hatia, ikiwa hana hatia, mchezo unaisha, ataachiwa huru, ikiwa amepatikana na hatia hatua nyingine itafuata.

(i) Sababu za kupunguziwa adhabu.

Wakati mshitakiwa anahukumiwa, upande wa utetezi utapewa nafasi ya kuwasilisha hoja ambazo zitapunguza adhabu na upande wa mashitaka utapewa nafasi kuwasilisha hoja ambazo zitaongeza adhabu.

(j) Hukumu

Hili litakuwa jambo la pili kutoka mwisho, mahakama itasoma hukumu ndani ya siku 90 kwa mujibu wa kifungu cha 311 cha Sheria ya Mwenendo wa Makossa ya Jinai. Mfumo wa hukumu umetolewa chini ya kifungu namba 312 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.

(k) Ufafanuzi Kuhusu Haki ya Kukata Rufaa

Jaji / hakimu lazima aieleze haki ya kukata rufaa kwa upande wowote ambao haujaridhika na hukumu ya mahakama. Zingatia sheria ya siku sitini iliyopo chini ya kifungu cha 225 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambacho kinahitaji upelelezi wa jinai kukamilika ndani ya siku 60 tangu siku ya kuanza isipokuwa kwa baadhi ya makosa mengine makubwa ambayo uchunguzi wake unaweza kuwa wa muda mrefu kama uasi.

Sura ya

8

Kuboresha Ulinzi Ofisini na Nyumbani

8.0 Utangulizi

Usalama katika makao makuu ya shirika au ofisi na katika nyumba za wafanyakazi ni muhimu sana kwa kazi ya watetezi wa haki za binadamu. Muongozo huu unaeleza kwa kina kuhusu jinsi usalama wa ofisi au nyumba inavyoweza kuchambuliwa na kuboreshwa.

8.1 Mambo ya jumla kuzingatiwa katika usalama wa ofisi

Malengo ya kuboresha usalama yanaweza kufupishwa kwa kutumia maneno yafuatayo:

- Kuzuia upatikanaji wa taarifa usio idhinishwa. Katika visa vidogo pia ni lazima kulinda ofisi dhidi ya mashambulizi yanayoweza kutokea (dhidi ya mabomu).
- Udhaifu wa ofisi. Huu unaongeza hatari, kulingana na tishio unalokabiliana nalo. Kwa mfano, ikiwa upo katika hatari ya kuibiwa vifaa au taarifa, lazima uondoe udhaifu huo kwa usahihi. Kengele ya usiku itakua na umuhimu mdogo ikiwa hakuna mtu anayekuja na kuangalia kilichotokea. Kwa upande mwingine, ikiwa kuna vurugu mchana, fensi iliyoimara kwenye mlango au kengele haitakuwa muhimu sana. Kwa kifupi, chukua hatua kulingana na vitisho ambavyo unakumbana navyo na namna unavyovishughulikia.
- Udhaifu wa ofisi lazima upimwe kulingana na vitisho unavyoweza kukabiliana navyo. Hata hivyo, ni muhimu kuweka usawa katika kuchukua hatua sahihi za usalama na kutoa hisia kwa watu wa nje kwamba kuna kitu “kimefichwa” au “kulindwa”. Kwa sababu hii inaweza kukuweka katika hatari. Katika usalama wa ofisi mara nyingi unapaswa za kawaida, hatua ambazo ni za dhahiri zaweza kuchukuliwa ikiwa ni lazima.
- Usalama wa ofisi sio mkubwa kuliko sehemu yake dhaifu. Ikiwa mtu anataka kuingia bila wewe kufahamu, hatachagua njia ngumu zaidi ya kuingia ili kufanya hivyo. Kumbuka kuwa njia rahisi ya kuingia ofisini na kujionea kinachoendelea ndani wakati mwingine ni kubisha mlango na kuingia ndani.

8.2 Mahali pa kuweka ofisi

Mambo ya kuzingatia wakati wa kutafuta mahali pa kuweka ofisi ni:

- Majirani; ikiwa jengo linahusishwa na watu fulani au shughuli fulani za zamani;
- Upatikanaji wa usafiri wa umma na binafsi;
- Hatari ya ajali;
- Jinsi gani jengo linafaa kuweka hatua muhimu za usalama, nk.

Ni muhimu kufanya mapitio ni hatua gani za usalama zinazochukuliwa na wengine katika maeneo jirani. Ikiwa zipo nyingi, hii inaweza kuwa ishara ya eneo kuwa sio salama, kwa mfano, kuhusiana na makosa ya kawaida. Pia ni muhimu kuzungumza na watu katika eneo hilo juu ya hali ya usalama wa eneo husika. Kwa hali yoyote, hakikisha hatua za usalama zinaweza kuchukuliwa bila kuvutia hisia zisizofaa za watu. Pia ni muhimu kujua watu jirani sababu wanaweza kukupatiaa habari kuhusu tuhuma yoyote inayoendelea kwa jirani.

Pia ni muhimu kuangalia ni nani aliyekupangisha. Je, sifa zao ni zipi? Je, wanaweza kuwa na shinikizo kutoka kwa wenye mamlaka? Je! Watakuwa na amani na wewe kuweka hatua za usalama?

Uchaguzi wa ofisi lazima uzingatie nani ambaye anahitaji kuja ofisini. Ofisi ambayo waathirika wanakuja kutafuta ushauri wa kisheria itakuwa na mahitaji tofauti na ofisi ambayo ni maalumu kwa wafanyakazi pekee. Ni muhimu kuzingatia jinsi ambavyo ni rahisi kufikia usafiri wa umma, itakuwa na safari iliyo salama kati ya eneo ambako wafanyakazi wanaishi, ambapo kazi nyingi hufanyika, nk. Maeneo ya jirani yanapaswa kufanyiwa tathmini, hasa ili kuepuka kusafiri katika maeneo ambayo sio salama.

Mara tu eneo likishachaguliwa, ni muhimu kufanya tathmini za mara kwa mara za eneo ambalo linaweza kutofautiana, kwa mfano, kama ‘kipengele kisichohitajika’ kinaingia kwa jirani.

Orodha ya mambo muhimu kuzingatia unapochagua eneo la kuweka Ofisi

UJIRANI:	Takwimu za uhalifu; ukaribu na maeneo yaliyolengwa kwa mashambulizi ya silaha, kama vile mitambo ya kijeshi au serikali; kuhakikisha usalama maeneo ya kujihifadhi; mashirika mengine ya kitaifa au ya kimataifa ambayo una uhusiano nayo.
MAHUSIANO:	Aina ya watu katika ujirani; mmiliki / mpangishaji, wapangaji wa zamani; matumizi ya zamani ya jengo hilo.
UPATIKANAJI:	Njia moja au njia nyingi nzuri za usafiri (nyingi zaidi, ni bora zaidi); upatikanaji wa usafiri wa umma na binafsi.
HUDUMA ZA MSINGI:	Maji, umeme na simu
MWANGA KATIKA MTAA:	Katika eneo jirani
VIASHIRIA VYA AJALI AU HATARI ZA ASILI:	Moto, mafuriko mazito, maporomoko ya ardhi, kutupa vifaa vya hatari, viwanda vilivyo na michakato inayosababisha madhara, nk.

MUUNDO WA NJE:	Uimara wa miundo, kituo kwa ajili ya kufunga vifaa vya usalama, milango na madirisha, mzunguko na vikwazo vya ulinzi, pointi za kufikia (tazama hapa chini).
VYOMBO VYA MOTO VYA USAFIRI:	Karakana au angalau maegesho ya magari

7.3 Mambo mengine muhimu ya kuzingatia kuboresha usalama nyumbani na ofisini;

(a) Uzio ikiwa ni pamoja na uzio wa umeme. Ni muhimu kwamba ambapo rasilimali inaruhusu, ofisi za Watetezi wa Haki za Binadamu zinapaswa kuwa na uzio na pale inapowezekana, zinapaswa kuwa na uzio wa umeme.

(b) Vifaa vya ofisi na mafunzo (sanduku la huduma ya kwanza, zima moto mafunzo ya mara kwa mara ya namna ya kuzitumia. Tumia pia namba za milio ya bure.

(c) Funguo za Ofisi hazipaswi kuwa sehemu ya wazi hasa kwa wageni. Zinapaswa kuwa sehem ambapo watu wachache wanaweza kuziona. Fanya mabadiliko ya mara kwa mara ya neon la siri kwa usalama.

(d) Ukiwa unatoka ofisini kwako, hata ikiwa ni kwa dakika chache, hakikisha unafunga kompyuta yako na kulinda hati zako za siri ili watoto na wavamizi wasizifikie kwa urahisi. siojiunga wawe rahisi kufikia. Hakikisha kwamba milango ya ofisi na baraza imefungwa, iwe upo ndani au nje ya ofisi. Kabla ya kuondoka ofisini kwako kila siku, hakikisha unasafisha dawati lako na uondoe hati yoyote. Pia, hakikisha unafunga madirisha yako, kabati za faili na dawati.

(e) Wekea alama Vifaa vya Ofisi yako. Hakikisha unawekea alama vifaa vya ofisi yako na alama za kitambulisho (ID), mihuri au stika na idadi yako ya hesabu na nembo.

(f) Weka orodha kamili ya vitu vyote katika ofisi yako, mahali panapoonekana (hasa kwenye ukuta wa ofisi), ili wewe na wafanyakazi wako waweza kuhakikisha wakati wowote kwamba kila kitu kiko katika mahali pake.

(g) Vaa beji za kitambulisho. Hakikisha wafanyakazi wako wote wana majina yao yameandikwa kwenye beji zao za utambulisho. Zaidi, wateja wa ofisi wanapaswa kupewa beji za utambulisho wa wageni. Hii ni kipimo kikubwa cha usalama ambacho unaweza kutumia kwa faida yako. Kwa hiyo, unaweza kujua nani anayekuja au kwenda nje ya eneo lako la ofisi.

(h) Sakinisha mifumo ya CCTV. Faida za mifumo ya CCTV ni nyingi. Inatumika kama mwongozo kwa wafanyakazi wako na pia njia ya kukamata wahusika au wahalifu katika ofisi yako. Kufunga mifumo ya CCTV ni mojawapo ya njia rahisi zaidi na za ubunifu za kuongeza usalama katika ofisi yako. Ikiwa unataka kuimarisha usalama wa ofisi yako au mahali pa kazi, hakikisha unaweka CCTV katika karakana na mlango wa kuingia katika ofisi yako.

(i) Wekeza katika mifumo ya miito ya sauti. Njia bora zaidi ya kuimarisha usalama wa ofisi yako ni kwa kuongeza mifumo ya miito ya sauti. Faida ni sawa na ufungaji wa kamera za CCTV mahali pa kazi. Kufunga mifumo ya miito ya sauti itafanya kazi kama kizuizi, mara tu watu wakiona eneo linalindwa na silaha ya miito ya sauti, watakuwa makini jinsi wanavyoingia na kwenda nje ya mahali hapo. Uzuri wa mifumo ya miito ya sauti ni kwamba itaonya mamlaka kama kuna kiashiria chochote cha shughuli za uhalifu, na wavamizi au wezi wataepuka kuja ofisini kwako.

(j) Weka Nywila zako Binafsi. Hakikisha beji zako za utambulisho, funguo, nywila za kompyuta, na kadi za muhimu ni zipo sehem salama. Unaweza kufanya hivyo kwa kuhakikisha humpi mtu ambaye huwezi kumwamini. Ikiwa inawezekana kwako, hakikisha usiitoe mara ya kwanza. Kuna watu ambao utawapa kwa uaminifu, na watatumia upendeleo huo vibaya,

(k) Jua ujirani wako. Unajua majirani zako na ujirani wako? Wahalifu mara nyingi zaidi kabla ya kuamua wapi na wakati gani wa kuingia na kufanya uhalifu, huangalia wakati gani wewe na familia yako huwa mnakuja na kuondoka. Kujua jirani yako na watu wanaoishi karibu na wewe itasaidia kuona wanaohusika au kutiliwa mashaka. Majirani zako wanaweza kuwa mstari wa kwanza wa ulinzi dhidi ya uvamizi nyumbani kwako wakati usipokuwepo. Wanajua eneo hilo na wanaweza kusaidia kutazama nyumbani kwako wakati uko mbali - lakini hawawezi kufanya hivyo ikiwa hawajui. Fanya jitihada za kukutana na majirani zako wapya na kuunda mahusiano mazuri ili uwe na watu wa kutegemea. Ikiwa kitu kibaya kinatokea katika eneo lako, jirani mwema atakufahamisha au kukujulisha. Kuzungumza na majirani zako kuhusu watu wanaotiliwa mashaka au magari yanayohusika.

(l) Mjue mpangishaji wako. Ikiwa mpangishaji atakubaliana na wewe kuweka vifaa vya usalama katika ofisi yako

(m) Weka mwanga juu ya maeneo yote yanayozunguka ofisi na nyumba yako.

Sura ya

9

Usalama Katika Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

9.0 Utangulizi:

Wewe ni Mtetezi wa Haki za Binadamu wa Kiafrika wa karne ya 21. Una silaha ya akili yako, hisia kali ya haki katika jamii, uhusiano na jamii za ndani, simu ya mkononi, skanu (iPad) na kompyuta mpakato. Miaka ishirini iliyopita vitu vitatu vya mwanzo vilikuwepo lakini simu ya mkononi na kompyuta mpakato ni vigeni katika karne ya 21. Teknolojia ya digitali inafanya uwezo wetu wa kutathmini hatari yetu ya kibinafsi na ya kitaaluma kuwa mgumu kwa sababu zinakuwa hazieleweki kwa urahisi. Bila ujuzi wa kitaaluma na kiufundi ni vigumu kutambua inapotokea vifaa hivyo vinavyohifadhi nyaraka nyeti vinapoziachia taarifa hizo kwa watu wengine. Pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015, Kanuni za Maudhui Mtandaoni 2018 (The Online Contents Regulations, 2018) ambayo kwa kiasi kikubwa ina vikwazo dhidi ya matumizi ya majukwaa ya mtandaoni kama barua pepe, Skype, Facebook Messenger, Instagram, Twitter, Whatsapp, youtube na kadhalika, ni muhimu kuwa salama unapokuwa mitandaoni.

9.1 Kuzungumza

Sio lazima taarifa ipitie kwenye mitandao ndipo itakapoweza kuchukuliwa na mtu mwingine kinyume cha sheria. Wakati wa kujadili masuala nyeti, fikiria mambo yafuatayo:

- Unawaamini watu unaozungumza nao?
- Je! Wanahitaji kujua taarifa unazowapa?
- Je! Uko katika mazingira salama? Vifaa vya kunasa mazungumzo au vifaa vingine vya kusikiliza mara nyingi hasa hupandikizwa katika maeneo ambapo watu hudhani kuwa ni salama, kama ofisi za faragha, mitaa yenye watu wengi, vitanda vya nyumbani na kwenye magari.

Inaweza kuwa vigumu kujua jibu la swali la tatu, kwa sababu vipaza sauti au vifaa vya kunasa sauti vinaweza kupandikizwa katika chumba kurekodi au kupeleka kila kitu kinachosema huko. Vinasa sauti pia vinavyotoa mwanga vinaweza kuelekezwa kwenye madirisha kutoka umbali mkubwa ili kusikiliza kile kinachosemwa ndani ya jengo. Mapazia mazito hutoa ulinzi dhidi ya vinasa sauti vinavyotoa mwanga (laser bugs), kama vile kufunga madirisha mara mbili na vioo. Baadhi ya majengo salama yana seti mbili za madirisha zilizowekwa katika ofisi ili kupunguza hatari ya vifaa vya kunasa sauti vinavyotoa mwanga.

(a) Unaweza kufanya nini?

- Daima dhania kuwa kuna mtu anasikiliza ndani. Kwa mtazamo huo wa kuwa na hofu kiasi kidogo, unakua na uwezekano mkubwa wa kuwa makini wakati unapokuwa na masuala ya siri.

- Wataalamu maalum wa vinasa sauti wanaweza kutumika kuchunguza na kugundua vinasa sauti, lakini inaweza kuwa ni vigumu kuwapata. Pia, wakati mwingine wataalamu hao wanaweza wakawa wamehusika katika kuweka vinasa sauti vya awali. Wakati wa kuondoa vinasa sauti, wanaweza kufanikiwa kupata vifaa vichache na "vidogo" tu au si ajabu wakakosa chochote na kutangaza ofisi ziko safi".
- Wafanyakazi wote wa usafi wa ofisi wanaweza kuwa tishio kubwa la usalama. Wao huingia mara kwa mara katika ofisi yako na kusafisha pamoja na kuchukua uchafu wote kila siku. Wafanyakazi wote wanapaswa kuchunguzwa kwa makini kwa usalama na hii inapaswa kuwa muendelezo, kwani wafanyakazi wanaweza kuathiriwa baada ya kujiunga na shirika lako.
- Badilisha vyumba vya mikutano mara nyingi iwezekanavyo. Kadiri vyumba na maeneo ya mikutano unayotumia kujadili na kubadilishana habari yanapokua mengi, ndivyo rasilimali watu na vifaa zaidi vitatakiwa kutumiwa kusikiliza na kupata taarifa kutoka kwako.
- Jihadhari na zawadi zinazoletwa kwaajili yako, hasa zawadi zinazolengwa kukaa kwa muda mrefu kama vile kalamu ya gharama kubwa, beji, au zinazotumika katika ofisi yako, kama karatasi nzuri au picha kubwa. Aina hizi za vitu zimetumiwa katika siku za nyuma kusikiliza mazungumzo ya faragha ya watu.
- Fikiria kuwa sehemu fulani ya taarifa yako imeathiriwa wakati wowote. Unaweza kubadilisha mipango na lugha mara kwa mara, na kuwapa wasikilizaji wako vipande vipande tu vya habari halisi. Wakati mwingine jaribu kutoa maelezo ya uongo ili uone ikiwa kuna mtu yeyote anatumia au anaitikia.
- Kupunguza ufanisi wa kinasa sauti kinachotumia mwanga, jadili maswala nyeti ukiwa kwenye chumba cha chini au chumba kisicho na madirisha. Vifaa vingine vya kunasa sauti vinavyotumia mwanga vinaweza kushindwa kufanya kazi vizuri wakati wa mvua na mabadiliko mengine ya anga.
- Cheza sauti iliyorekodiwa bila kelele au wimbo maarufu kuingiliana na vifaa vya kunasa sauti. Teknolojia ya gharama kubwa tu inaweza kuchuja kelele ili kusikia mazungumzo.
- Maeneo mengi mapana yanaweza kuwa na manufaa na yenye madhara. Kufanya mkutano katika mahali ampapo watu wengi hawafiki hufanya iwe rahisi kuona ikiwa unafuatiliwa au unatazamwa, lakini inakuwa vigumu kuepuka kwa kuingia ndani. Makundi ya watu hufanya iwe rahisi kuunganisha, lakini ni ngumu sana kuonekana na kusikiwa.

(b) Simu za mkononi

Simu zote zinaweza kusikilizwa ikiwa msikilizaji ana uwezo wa kutosha wa teknolojia. Hakuna simu inayoweza kudhaniwa kuwa salama. Simu za mkononi za analojia si salama zaidi kuliko simu za mkononi za dijitali, na zote mbili sio salama zaidi kuliko simu za mezani.

Sehemu uliyopo na mazungumzo yako yanaweza kunaswa kupitia ufuatiliaji wa simu. Si lazima uwe unaongea na simu ili kufuatiliwa - hii inaweza kufanyika wakati wowote simu yako ya mkononi inapokua imewashwa.

Usihifadhi habari kama majina nyeti na namba kwenye kumbukumbu ya simu yako. Ikiwa simu yako imeibiwa, taarifa hizi zinaweza kutumika kufuatilia baadae na kuathiri watu unaotaka kuwalinda.

(c) Mambo ya msingi kuzingatia katika usalama wa kompyuta na faili

- Fungia kompyuta yako wakati wa kuondoka ofisini, kama inawezekana. Zima kompyuta yako unzpotoka.
- Tumia vifaa vya kuzuia kuongezeka kwa umeme (kupungua na kuongezeka kwa umeme kunaweza kuharibu kompyuta yako).
- Weka kitunza kumbukumbu, ikiwa ni pamoja na faili za karatasi, katika mahali salama na tofauti na mahali pa kawaida. Hakikisha vitunza kumbukumbu viko salama kwa kuviwekea nywila au kuviweka kwenye kompyuta inayolindwa na nywila za kisasa.
- Kupunguza hatari ya mtu kuingia kwenye kompyuta yako, linda kompyuta yako na mara zote zima kompyuta yako wakati wa kuondoka.
- Weka nywila kwenye faili zako ikiwa mtu anaweza kufikia kompyuta yako au pitia tena kuhakikisha ulinzi wako. Ikiwa kompyuta yako imeibiwa au kuharibiwa, utakuwa na uwezo wa kurejesha faili zako ikiwa umeweka ulinzi katika vitunza kumbukumbu (secure back-up) kila siku. Tunza nywila zako mbali na ofisi yako katika mahali salama. Faili zilizofutika haziwezi kurudishwa upya ikiwa umezifuta kwa kutumia kifutio cha PGP au huduma nyingine, badala ya kuziweka kwenye file la takataka la kompyuta (Recycle been).
- Kompyuta yako inaweza kupangiliwa katika hali itakayoifanya itume taarifa au faili zako kwa mtu mwingine na kukuweka katika hatari bila wewe kujua. Ili kuepuka hili, nunua kompyuta yako kutoka kwenye chanzo cha kuaminika, futa kila kitu kwenye kompyuta unapoinunua na kuanza kuitumia kwa mara ya kwanza, na kisha weka programu unayotaka. Tumia mafundi wa kuaminika kutoa huduma kwenye kompyuta yako na kuwaangalia wakati wote.
- Zingatia kuondoa uhusiano wa simu na kompyuta yako / modem, au vinginevyo zima muunganiko wa intaneti, unapoondoka kwenye kompyuta yako. Kwa njia hii, programu

zinazoletwa kwenye computer yako ili kukudhuru katikati ya usiku hazitafanya kazi. Usiache kompyuta yako ikiwa inawaka wakati unapoondoka. Jaribu kuweka programu ambayo italemaza au kuzuia upatikanaji wa taarifa katika kompyuta yako baada ya muda fulani inapokaa bila kutumiwa. Kwa njia hii, kompyuta yako haitakuwa hatarini wakati unapopata kahawa au kutoa nakala unapokua ofisini.

- Katika matumizi yako ya wavuti, fungua faili jipya ili uweze kujua ni aina gani ya faili kabla ya kulifungua. Hutakiwi kufungua virusi kwa kufungua faili ambayo ulifikiri ilikuwa faili ya maandishi. Katika Internet Explorer, nenda kwenye orodha ya vifaa (Tools) na chagua Chaguo za folda. Bonyeza "Angalia" (View) na uhakikishe kuwa sanduku la kuficha taarifa za nyongeza kwa taarifa zinazotambulika hazijaangaliwa.

(d) Mambo ya msingi kuzingatiwa katika Usalama wa Mtandao

Virusi na matatizo mengine, kama vile program zenye virusi, zinaweza kutoka popote; hata marafiki wanaweza kueneza virusi bila kujua. Tumia programu nzuri za kupambana na virusi (anti-virus) na uendelee kuziweka kumbukumbu mpya mara kwa mara ili ziweze kujiendesha zenyewe mtandaoni. Virusi wapya wanaundwa mara kwa mara na kugunduliwa, kwa hiyo angalia Maktaba ya Habari ya Virusi kwenye www.vil.nai.com kwa taarifa za virusi vya hivi karibuni na namna ya kujilinda navyo.

Virusi huenea kwa njia ya barua pepe, kwa hivyo fanya mawasiliano kwa barua pepe salama (angalia hapa chini). Virusi ni programu moja iliyoundwa ili kujizalisha na kuongezeka, inaweza iwe au isiwe mbaya. Programu zenye virusi kama "Trojans" zimeundwa kumfanya mtu wa tatu (au mtu yeyote!) aweze kuifikia kompyuta yako bila wewe kujua.

Anwani ya barua pepe inaweza kufungwa au kutumiwa na mtu mwingine mbali na mmiliki halali wa anuani hiyo. Hii inaweza kufanywa kwa kuingia katika kompyuta na nywila ya mtu mwingine, kwa kuvamia na kuiba, au kwa kutumia anwani inayoonekana kuwa anwani ya mmiliki husika. Kwa mfano, kwa kubadilisha helufi "l" na namba "1", unaweza kuunda anwani sawa na watu wengi hawatagundua tofauti.

Ili kuepuka kudanganywa, tumia mistari yenye maana na mara kwa mara uulize maswali ambayo mtu husika pekee ndiye atakayeweza kujibu;

- Hakikisha maombi yoyote ya taarifa unayoyatilia shaka unayafuatilia kwa njia nyingine ya mawasiliano.
- Weka shughuli zako unapopitia mtandao binafsi kwa kutokukubali kujirudia na kwa kufuta wavuti yako baada ya kila unapomaliza kutumia mtandao. Katika Internet Explorer, nenda kwenye 'Vifaa' (Tools), kisha 'Machaguo' (Options). Katika Netscape Navigator, nenda kwenye Hariri, kisha Mapendeleo. Wakati upo katika mojawapo ya sehemu hizi, futa historia yako yote uliyotumia katika mtandao. Kumbuka kufuta alama zako zote pia. Watazamaji pia

wanaweka kumbukumbu za tovuti unazozitembelea kwenye faili la taarifa zilizotembelewa, hivyo tafuta mafaili ambayo yanapaswa kufutwa kwenye mfumo wako.

- Boresha wavuti ili kuweka taarifa zako katika faili zenye nywila ili mtu asiyehusika asiweze kuziona. Hii itasaidia kulinda maelezo yoyote unayotaka kupitisha salama juu ya wavuti, ikiwa ni pamoja na nywila na data zingine nyeti zilizowasilishwa katika fomu. Weka programu ili kuboresha usalama wa program zote zilizotumiwa, hasa Microsoft Office, Microsoft Internet Explorer na Netscape.
- Usitumie kompyuta inayotumika kuhifadhi taarifa nyeti katika kupitia taarifa zisizo muhimu kwenye mtandao.

(e) Mambo ya muhimu kuzingatia katika usalama wa Barua Pepe

Haya ni mambo muhimu katika usalama wa barua pepe ambayo wewe na marafiki zako wote na washirika wako lazima mfuate ili kujihakikishia usalama wenu. Wajulishe kuwa hutafungua barua pepe zao isipokuwa kama watatuma taratibu za kiusalama.

- Usifungue barua pepe kutoka kwa mtu usiyemjua.
- Usiendelee kutuma kwa watu wengine barua pepe iliyotoka kwa mtu usiyemjua, au ambayo imetoka kwa mtu ambaye humjui. Barua pepe zote za “kuwa na mawazo ya furaha” ambazo watu hutumiana zinaweza kuwa na virusi. Kwa kuwatumia marafiki na washirika wako unaweza kuwa unawaambukiza virusi kwenye kompyuta zao. Ikiwa umeupenda ujumbe, uandike na ujitumie mwenyewe. Ikiwa kuuandika upya haina thamani ya muda wako, labda si ujumbe muhimu.
- Usipakue au kufungua kiambatisho isipokuwa unajua kinahusiana na nini na ambacho ni salama. Zima chaguzi za kupakua moja kwa moja katika programu yako ya barua pepe. Virusi vingi na programu huenea vyenyewe kama “minyoo” na vidudu vya kisasa mara nyingi huonekana kuletwa na mtu unayemjua. Vidudu vidogo vinachunguza kitabu chako cha anwani, hasa ikiwa unatumia Microsoft Outlook au Outlook Express, na ukaiga kwa kukijenga kama kiambatanisho muhimu kutoka kwa washirika halali. Saini barua pepe zako zote kwa kutumia programu ya PGP, hii inaweza kupunguza mchanganyiko zaidi wa virusi katika viambatanisho vyisivyo na virusi ambavyo unatuma kwa wenzako (PGP ni programu ya kuhifadhi taarifa, tafadhali angalia hapa chini)
- Usitumie lugha ya programu/viunganishi vya mtandaoni (HTML and MIME) katika barua pepe yako – tumia ujumbe wa kawaida. Barua pepe zenye viunganishi vya mtandaoni zinaweza kuwa na programu hatari zinazoweza huingilia na kuharibu faili zako za kompyuta.
- Ikiwa unatumia programu ya Outlook au Outlook Express, funga chaguzi za mapitio ya skrini (Preview screen options).

- Weka nywila kwenye barua pepe yako wakati wowote iwezekanavyo. Barua pepe ambayo haina nywila ni kama kadi ya posta ambayo inaweza kusomwa na mtu yeyote anayeiona au anayeipata. Barua pepe iliyofichwa ni kama barua katika bahasha ambayo ni salama.
- Tumia kichwa cha ujumbe chenye maana ili msomaji ajue kwamba ulilenga kutuma ujumbe. Waambie marafiki zako na wafanyakazi wenzako daima waandike kitu fulani katika kichwa cha ujumbe ili ujue kwamba ni kweli wao ndio waliotuma ujumbe. Vinginevyo mtu mwingine anaweza kuingilia mawasiliano yenu, au visusi aina ya 'Trojan' inaweza kutuma programu iliyo ambukizwa katika orodha yako yote ya barua pepe, ikiwa ni pamoja na wewe mwenyewe. Hata hivyo, usitumie vichwa vya ujumbe vinavyotoa taarifa inayotakiwa kuwa salama katika barua pepe zilizofichwa. Kumbuka, kichwa cha ujumbe hakifichwi kwa nywila na unaweza kutoa asili ya taarifa zilizohifadhiwa, ambayo inaweza kusababisha mashambulizi. Programu nyingi zinazotumika kuvamia mtandaoni siku hizi zinanakili moja kwa moja vichwa vya kuvutia vya barua pepe kama vile "ripoti", "siri" "binafsi" na vichwa vingine vinavyoonyesha kuwa ujumbe ni wa manufaa/muhimu.
- Kamwe usitume barua pepe kwenye kikundi kikubwa kilichoorodheshwa kwenye "To" au "CC". Badala yake, tuma ujumbe kwako mwenyewe na ujumuishe jina la kila mtu katika mistari "bcc". Hii ni njia bora na ya kawaida ya kutunza faragha.
- Kamwe usijibu barua pepe zilizokwenye faili la spam, hata kuomba kuondolewa kwenye orodha. Spam hutuma barua pepe kwenye orodha ya barua pepe nyingi zilizojificha na hazijulikani ni zipi zinazotumika- inamaanisha kuwa mtu anatumia anwani ya barua pepe kikamilifu. Kwa kujibu, seva inakutambua kama uko "hai" na utakuwa na uwezekano wa kupokea spam nyingi zaidi.
- Ikiwezekana, tunza kompyuta tofauti, usiounganishwa na nyingine yoyote, ambayo inakubali barua pepe za jumla na haina faili za data.

(f) Vidokezo vya jumla kwa watoa huduma za internet na zaidi

Barua pepe zilizotumwa bila maandishi au zisizojulikana kwenye mtandao zinaweza kusomwa na watu wengi zaidi, ikiwa wakifanya jitihada za namna hiyo. Mojawapo ya haya inaweza kuwa Mtoa huduma wa Internet wa ndani (ISP) au ISP yoyote ambaye barua pepe zako zinapita. Barua pepe inasafiri kupitia kompyuta nyingi ili kutoka kwa mtumaji kwenda kwa mpokeaji; inapita mipaka ya kijiografia na inaweza kupita kwenye seva za nchi nyingine hata kama unatuma barua pepe ndani ya nchi moja.

Baadhi ya vidokezo vya jumla juu ya masuala ya kawaida ambayo hayaeleweki kwa watumiaji wa internet:

- Nywila-inayolinda faili inatoa mchango mdogo sana kulinda faili ambayo haifai kufanya kwa nyaraka zenye taarifa nyeti. Inatoa tu maana ndogo ya usalama.

- Kufunga faili haizuii mtu kuangalia kilichopo ndani ya faili.
- Ikiwa unataka kuthibitisha faili au barua pepe imetumwa kiusalama, tumia programu maalumu ili kuruhusu wahusika tu kuona taarifa hizo (angalia www privaterra.com).
- Ikiwa unataka kutuma barua pepe au hati kwa usalama, tumia njia ya kuifunga kuanzia mwanzo hadi itakapofika kwa mpokeaji wa mwisho. Haifai kutuma barua pepe iliyofungwa kutoka ofisi ya kazi hadi New York au London au mahali pengine na kisha kuruhusu barua pepe hiyo itumwe bila kufichwa/kufungwa kwenda kwa mtu mwingine.
- Mtandao ni wa kidunia kiasili. Hakuna tofauti kati ya kutuma barua pepe kati ya ofisi mbili huko Manhattan na kutuma barua pepe kutoka kwenye café ya internet huko Afrika Kusini hadi kwenye kompyuta ya ofisi ya London.
- Tumia programu ambayo watu husika tu wanaweza kufikia data kwenye kompyuta (encryption), hata kama barua pepe au data unayotuma sio nyeti!
- Hakikisha kompyuta unayoyotumia ina programu ya ulinzi wa virusi. Virusi vingi vimeandikwa ili kuchukua taarifa kutoka kwenye kompyuta yako, ikiwa ni maudhui yako au faili zako za barua pepe, ikiwa ni pamoja na vitabu vya barua pepe.
- Hakikisha programu yako imeidhinishwa vizuri. Ikiwa unatumia programu ambazo hazijaizinishwa, unakuwa mdukuzi wa programu badala ya kuwa mwanaharakati wa haki za binadamu machoni mwa serikali na vyombo vya habari. Chaguo bora ni kutumia programu ya chanzo wazi - ni bure!
- Hakuna suluhisho la usalama wa asilimia mia moja ikiwa unatumia mtandao. Jihadhari kwamba mtu anaweza “kudukua kijamii” katika mfumo kwa kujifanya kuwa mtu asiyekuwa kwenye simu au kwa barua pepe. Tumia uelewa wako mwenyewe na akili ya kawaida.

(g) Mambo mengine muhimu:

- Daima hifadhi barua pepe zako katika fomu iliyofichwa (encrypted). Unaweza daima kuifichua (decrypt) tena baadaye, lakini ikiwa mtu anayo kompyuta yako, ni hatari zaidi kama haijawahi kufichwa.
- Uendelee na kila mtu ambaye mnatumiana barua pepe zilizofichwa ili uhakikishe kuwa hawafichui na kupeleka barua pepe, au kujibu bila kujisumbua kuzificha. Uvivu binafsi ni tishio kubwa katika mawasiliano yako.
- Huenda ungependa kuunda akaunti za barua pepe salama kwa watu wanaojifunza kwa vitendo, ambazo hazitumiwi kwa kawaida na hivyo hazichukuliwi na seva za spam. Anwani hizi zinapaswa kuchunguzwa mara kwa mara lakini hazitumiwi, ila kwa wafanyakazi wanaojifunza kwa vitendo. Kwa njia hii unaweza kuharibu anwani za barua pepe ambazo zinapata spam nyingi bila kuhatarisha msingi wako wa mawasiliano.

(h) Internet na sheria

Kufuatia kutungwa kwa Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015, Kanuni za Maudhui ya Mtandao, 2018 na Sheria ya Huduma za Vyombo vya habari, 2016, mawasiliano yamezuiliwa kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo ni muhimu kwa mtetezi wa haki za binadamu kuhakikisha;

- Kamwe husambazi na / au kutuma ujumbe kwenye vyombo vya habari vyovyote vya kijamii ambavyo hauna uhakika wa uhalali wake. Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015 ipo daima kukunasa mara moja unapoikiuka.
- Weka mawasiliano yako salama. Unaweza kupakua programu ya bure inayojulikana kama Automatic Call Reccorder moja kwa moja kwenye simu ili kurecodi mawasiliano yako yote na kukusaidia katika marejeo ya baadaye.
- Epuka kusambaza video za ngono au picha nyingine yoyote ya ngono
- Epuka kutumia lugha ya matusi kwenye vyombo vya habari vya kijamii
- Hupaswi kuendesha jukwaa lolote la mtandaoni ambalo linatakiwa kusajiliwa lakini haujasajili.

KUMBUKA: Yaliyopo hapo juu sio orodha kamili ya kile ambacho haupaswi kufanya, watetezi wa haki za binadamu wanahimizwa kutafuta muda na kupitia sheria zilizoelezwa hapo juu kwa ajili ya marejeo yao na kuongeza ufahamu.

Sura ya

10 Kutathmini Utendaji wa Usalama wa Shirika

10.0 Utangulizi

Kama shirika, kuna uwezekano kwamba tayari kuna hatua za usalama zilizopo. Wakati huo huo labda huhisi kama kuna nafasi ya kuboresha – kawaida ni Kujua ni wapi pakuanzia. Inaweza kuonekana kuwa kubwa sana kwa hivyo ni wazo nzuri kufanya tathmini ili kupata maelezo ya kweli ya usalama wa shirika uliloanzisha.

Kuna watu muhimu ambao wanapaswa kuingizwa katika mchakato huu. Hizi zinaweza kutofautiana shirika na shirika na inaweza kuwa na manufaa kuingiza washauri wa nje ili kusaidia kuongoza mchakato pia. Kwa mfano:

Ndani - Bodi ya wakurugenzi, mkurugenzi mtendaji, wafanyakazi wa ngazi za juu, wafanyakazi wa kawaida na wakujitolea.

Nje - Waajiri, washauri wa nje na wakufunzi

Kuhusisha kila mmoja wa watendaji hawa kuna manufaa na hasara na ni muhimu kwamba mchakato unafanywa kwa njia ya umoja, shirikishi, uwazi na isiyo ya kuhukumu. Mpangilio rasmi ndani ya mashirika unahitaji kubaki nyeti kwa mahitaji ya programu yao na wafanyakazi wanaojifunza kwa vitendo au wakujitolea ambao wanaweza kukabiliwa na hatari kubwa katika kazi zao za siku hadi siku. Wafanyakazi na wanaojitolea wanapaswa pia kuheshimu ukweli kwamba usimamizi unakabiliwa na kazi ngumu katika kusimamia njia ya usalama.

10.1 Vigezo vya tathmini

Tunaweza kuanza kwa kuangalia masuala na viashiria vyenye uhalisia ili kusaidia kuchunguza jinsi taratibu za usalama zinazingatiwa na wafanyakazi. Zingatia pointi zifuatazo:

- Uzoefu wa usalama uliopatikana: Je, wafanyakazi wana uzoefu wa kutekeleza utendaji wa usalama? Je! Uzoefu huu umeenea sawasawa kwa wafanyakazi, au kujilimbikizia kati ya watu wachache?
- Mafunzo ya usalama. Mafunzo ya Usalama kupitia kozi au kupitia mpango wa watu binafsi wakati wa kazi za kila siku. Rasilimali, muda na nafasi zinahitajika kupatikana kwa mafunzo (ama rasmi au yasiyo rasmi). Je, mafunzo hayo yanapatikana kwa wanachama wa shirika? Je hii inajumuisha mafunzo juu ya ustawi wa kisaikolojia na kijamii na usalama wa kidijitali?

- Mtazamo na ufahamu: Je, watu wanafahamu umuhimu wa usalama na ulinzi? Je! Mtazamo wao juu yake ni chanya na wazi kufanyiwa maboresho? Je! Wanajua vikwazo gani wanavyokumbana navyo? Je, mtazamo na uelewa kuhusu usalama wa dijitali, usalama wa nje na ustawi wa kisaikolojia wa jamii unagawanywa katika shirika?
- Mpango wa Usalama: Mpango wa usalama unahusiana na kazi zinazofanywa? Ni mara ngapi uchambuzi wa mazingira umefanywa na mpango ya usalama umeundwa? Je! Mipango inapitiwa mara kwa mara, na inajumuisha usimamizi wa vifaa vya dijitali?
- Mgawanyo wa kazi na majukumu: Je, Kuna mgawanyo wa wazi wa majukumu ya utekelezaji wa mpango wa usalama wetu? Je, majukumu haya yamezingatiwa kwa kiasi gani, na ni vipi vikwazo vinavyoonekana?
- Umiliki na kufuata sheria: Watu wanahusikaje katika mpango wa usalama wa shirika, na kwa kiwango gani wanazingatia mipango iliyopo? Je, ni matatizo gani yanayotokea hapa, na yanaweza kusuluhishwa? Je Mchakato unaweza kufanywa shirikishi zaidi?
- Majibu ya matukio ya usalama: Ni mara ngapi matukio ya usalama yanagawanywa kwa watu? Ni mara ngapi yanachambuliwa na hatimaye kufanyiwa kazi ikiwa kunaulazima?
- Tathmini ya mara kwa mara: Mikakati na mipango ya usalama hupangwa mara ngapi? Je, kuna mchakato mahususi kwa ajili ya hili, au in ategemea na mazingira? Inawezekana kufanywa mara kwa mara au zaidi? Je matatizo gani yanayojitokeza na yanawezaje kutatuliwa?

10.2 Gurudumu la Usalama

Ufuatiliaji wa usalama wa shirika kwa kutumia vigezo sawa unaweza kutekelezwa kwa kuzingatia gurudumu la usalama na sehemu zake nane. Mantiki ni kwamba gurudumu lazima liwe na usawa pande zote ili liweze kuzunguka; kwa maneno mengine, sehemu zote zinahitajika kuwa za urefu sawa. Hali hiyo inatumika katika gurudumu la usalama na sehemu zake 8 (vipengele) vinavyowakilisha usimamizi wa usalama katika shirika au kikundi cha watetezi.

Tathmini hii inaweza kufanyika kwa makundi ya watendaji wote katika shirika kama ifuatavyo:

i. Chora Mchoro wa gurudumu
ii. Jaza nafasi kila sehemu kulingana na jinsi unavyofikiri ni sahihi na halisi
iii. Andika sababu (tafakari) kwa nini baadhi ya sehemu maalum zimejazwa kidogo kulinganishwa na sehemu zenye ujazo mkubwa, orodhesha njia ulizotumia kufikia matokeo hayo na kuweka malengo na taratibu husika na kuonyesha ufumbuzi.
iv. Mara baada ya kumaliza zoezi hili, tunza salama nakala ya gurudumu lako na rudia zoezi baada ya miezi michache. Utakuwa na uwezo wa kulinganisha magurudumu mawili na kuamua uhakika na hatua ikiwa mambo yamebadilika.

Sampuli ya gurudumu la usalama

Gurudumu la usalama ni nadra kuwa kamilifu: Vipengele vingine vinaujazo zaidi kuliko vingine. Kwa hiyo ni muhimu kuamua kiwango cha ujazo wa kila sehemu. Kwa njia hii, unaweza kutambua ni mipango gani ambayo inahitaji kupitishwa ili kuboresha ulinzi na usalama wako na shirika.



Chora gurudumu kwenye chati, paka rangi kwenye sehemu za ndani kuelezea sura halisi ya gurudumu kwa kundi lako au shirika. Basi utaweza kwa urahisi kuona vipengele ambavyo vimejazwa zaidi -na ambavyo vimejazwa kwa kiwango cha chini.

Sura ya

11

Kuunda na Kutekeleza Mpango wa Usalama

11.0 Utangulizi

Mpango wa usalama ni hati ambayo inajumuisha hatua za kinga na kukabiliana na masuala yote ya usalama na ulinzi ambayo huimarisha ulinzi na usalama binafsi na wa shirika. Huu ni mpango na mkakati wa ulinzi na usalama wa shughuli zote za shirika, wafanyakazi, na wadau wengine.

11.1 Tofauti kati ya Sera ya Usalama na Mpango wa Usalama.

Sera ya usalama ni jumla ya kanuni na miongozo ndani ya shirika ili kukidhi mahitaji ya usimamizi sahihi wa usalama. Mpango wa usalama unaweza pia kuzingatia utekelezaji wa sheria, kanuni, na miongozo hiyo kwa lengo la kuendana na hali husika katika kipindi fulani au shughuli fulani inayofanywa na shirika. Kwa mfano, shirika linaweza kuunda mpango wa usalama huku likijitayarisha kwenda kwenye uchunguzi kwa vitendo na kuweka kanuni au sera zinazolenga kushughulikia na kuangalizia suala la usafiri wa wafanyakazi na usalama wao.

11.2 Watetezi wa Haki za Binadamu na mipango ya ulinzi na usalama Tanzania.



Kwa mujibu wa ripoti ya THRDC ya 2013 juu ya tathimini ya mahitaji ya ulinzi na usalama, ni mashirika manne tuu ya haki za binadamu kati ya mashirika 200 yaliyoshiriki katika tathmini hii ndiyo yaliyokuwa na Sera ya ulinzi na usalama pamoja na mipango iliyoandaliwa vyema, kanuni, sheria na majukumu mashirika hayo manne yalikuwa Action Aid Zanzibar, Care international Mwanza, OXFAM -Arusha na DONET huko Dodoma.

Mchoro hapo juu unaonesha mashirika ya haki za binadamu 196 yaliyotathiminiwa kuwa hayana Sera ya ulinzi na usalama au mpango wowote unaohusu usalama wao. Hadi wakati ambao Muongozo huu wa usalama na ulinzi unaandikwa, zaidi ya mashirika 10 ya utetezi wa haki za binadamu yana Sera ya ulinzi na mipango. Baadhi ya mashirika hayo ni Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Mtandao wa Programu ya Jinsia Tanzania (TGNP), Shirika la Kutetea hazi za watu wenye ualbino (UTSS), Mtandao wa kushughulikia masuala ya uzazi na madhara ya utoaji mimba usio salama (CAMMAC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kwa kutaja machache kati ya yote.

11.3 Namna ya kuunda Mpango wa Usalama.

Ili kuandaa mpango wa usalama, wafanyakazi wanapaswa kukutana na kutoa mawazo yao kupitia majadiliano ya pamoja ya usalama. Kama mmekwishafanya tathimini ya hali ya hatari katika Shirika lenu, mtakuwa tayari mmeweza kufahamu orodha ndefu ya mambo hatarishi, hofu, woga, wasiwasi aina kadha ya vitisho na orodha ya njia za kukabiliana navyo.

i. Chagua vitisho vichache.

Panga kwa orodha ya vitisho hivyo kwa njia ya vipaumbele au viweke kwa mpangilio na daraja kufuatia uzito wake, tumia moja ya vigezo hivi: Vitisho vikali zaidi vya kutishia kifo, kwa mfano;

Hali ya kuweza kutokea vitishio vikubwa zaidi na vikali - ikiwa mashirika sawa na yako yameshambuliwa, hilo ni tishio la wazi na la kipaumbele katika chaguo lako; au tishio ambalo limetokea katika shirika sawa na lako na linatoa wasiwasi na hofu kama iliyokatika shirika lako sababu ya kuwa na wewe upo katika hali hatarishi kutokana na uwepo wa tishio la namna hiyo.

ii. Orodhesha

Wasiwasi, hofu ambazo zinatokana na vitisho ambavyo umeviorodhesha.

Hofu na wasiwasi vinapaswa kushughulikiwa kwanza, lakini kumbuka kuwa sio wasiwasi na hofu zote zinahusiana na vitisho vyote. Kwa mfano; ikiwa unapata au kupokea vitisho vya kifo, inaweza kuwa sio muhimu sana kuanza kukarabati, kuimarisha na kulinda kabati lako la ofisi ili kuzuia uvamizi katika ofisi yako iliyo katikati ya jiji (isipokuwa kama unaweza kushambuliwa kwa urahisi katika ofisi, ambayo sio kawaida).

Bali inaweza kuwa muhimu zaidi kwa kupunguza kukaa na kutembea bila ulinzi hasa wakati wa kutoka nyumbani kwenda ofisini au siku za mapumziko. kulinda na kuimarisha makabati ya ofisini yanayotumika kuhifadhia nyaraka sio kwamba sio muhimu ni muhimu pia ila hii haitapunguza hofu na wasiwasi wako ya vitisho vya kifo unavyopokea.

(iii) Orodhesha uwezo wa utatuzi ambao unao wenye kuhusiana na vitisho ulivyo viorodhesha.

Sasa utakuwa katika nafasi ya kupambana vitisho vilivyo orodheshwa, wasiwasi, hofu na uwezo wa utatuzi na kukabiliana katika mpango wako wa usalama, na kwa namna hiyo inawezekana kabisa kwamba utapunguza hali yako hatarishi kupitia njia hizi.

Tafadhali, fahamu kwamba hii ni njia moja ya haraka au ya ziada ya kuandaa mpango wa usalama. Kuna njia rasmi nyingi za kuandaa mpango wa usalama ila mbinu hii ni rahisi na ya kueleweka na ina hakikisha una fanyia kazi masuala nyeti kwa haraka na usalama. Inafanya thamini yako ya hatari kuwa sahihi, na mwisho kuishia kukupa mpango imara na halisia, ambao ndio sehemu muhimu ya usalama.

11.4 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA USALAMA.

Mipango ya usalama ni muhimu ,ila sio rahisi kuitekeleza .utekelezaji wake ni zaidi ya mchakato wa kimbinu (technical process),ni mchakato wa kitaasisi, kishirika na kijumuiya na unahitaji uhusishaji na ushirikishwaji wa wafanyakazi wote,na uungwaji mkono wa menejimenti yote ya shirika. Pia unahitaji uwepo wa mawasiliano miongoni mwa wote waliohusishwa katika uandaaji wake kwa mujibu wa maudhui. Kuwe na hatua za kuhakikisha nia ya dhati ya utekelezaji, kuipitia mipango hiyo mara kwa mara ili iendane na wakati husika.

Hii ina lengo la kutafuta mkakati, fursa na vikwazo na matatizo katika mipango hiyo ya usalama wakati wa utekelezaji.

- Mpango usalama unapaswa kutekelezwa katika ngozi kuu tatu.
  i. Ngazi ya mtu mmoja mmoja. Kila mtu ana takiwa kufuata mpango usalama ili uweze kufanya kazi.
  ii. Ngazi ya shirika. Shirika lote kwa ujumla linatakiwa kufuata mpango huo.
  iii. Ngazi ya Shirika na Shirika

Hii hutokea pale ambapo shirika na shirika linaingia ushirikiano miongoni mwao mpango wa usalama mara nyingi ni muhimu pia kuuhusisha ili kulinda usalama.

Mifano ya mikakati na fursa wakati wa utekelezaji wa mpango wa usalama;

- Pale ambapo suala dogo la kiusalama limetokea katika shirika lako au shirika lingine na wafanyakazi wanaingiwa na hofu hii hufanya wazidi kuwa makini zaidi.
- Kutokea kwa suala linalohusu usalama kwa ujumla kutokana hali fulani ilivyo nchini.
- Mfanyakazi mpya anayeanza kazi anaweza kufundishwa kuanza masuala ya usalama vizuri na kwa urahisi zaidi.
- Shirika lingine linapokupa msaada wa mafunzo ya usalama.

Mifano m ya matatizo na vikwazo wakati wa utekelezaji wa mpango wa usalama.

- Watu hudhani kuchukua hatua za kiusalama zitapelekea mzigo wa majukumu katika shirika.
- Wengine hufikiri huwa shirika tayari lina usalama na ulinzi wa kutosha.
- Wengine wamejikita katika shughuli zao na kupuuzia masuala ya usalama.

Hudhani kuwa mambo ya usalama sio kwaniaba ya shirika ila ni kwa niaba ya watu wanao kusudiwa kusaidiwa.

Sura ya

12

Usalama na Namna ya Kudhibiti Msongo wa Mawazo

12.0 Utangulizi.

Mara nyingi kwenye sehemu ya kazi mawazo na huzuni ni kawaida. Mawazo na huzuni kupita kiasi zinaweza kuingilia utendaji wako na uwezo wako kazini, huathiri afya yako ya kimwili na ya kihisia, na kuathiri mahusiano yako na maisha ya nyumbani. Inaweza hata kumanisha tofauti kati ya mafanikio na kushindwa katika utendaji wa kazi. Huwezi kudhibiti kila kitu katika mazingira yako ya kazi, lakini hiyo haimaanishi kuwa hauna uwezo wa kuzuia wakati unakabiliwa na hali ngumu na matatizo.

Kwa hali yeyote ya matakwa yako au mahitaji ya kikazi, kuna hatua ambazo unaweza kuchukua ili kujilinda kutokana na madhara mabaya ya huzuni na mawazo, kuboresha ufanisi wa kazi yako, kuimarisha ustawi wako ndani na nje ya kazi. Watetezi wa Haki za Binadamu kama kundi lolote la watu wanakabiliwa na mawazo na huzuni kwa sababu ya kazi zao. Kwa hiyo muongozo huu utasaidia mbinu za kupunguza na / au kuzuia mawazo na huzuni kwa watetezi.

12.1 Ni wakati gani mawazo na huzuni hutamalaki sehemu ya kazi?

Kuwa na mawazo sio jambo baya mara zote. Mawazo kidogo yanaweza kukusaidia kukaa kwa umakini, kuwa na nguvu, na uwezo wa kukabiliana na changamoto mpya mahali pa kazi.

Ndicho kinacho kupa umakini wakati wa uwasilishaji au tahadhari ili kuzuia matukio yenye madhara, ajali au makosa makubwa. Lakini katika dunia ya leo yenye hekaheka mahali pa kazi mara nyingi huonekana kama sehemu yenye kuongeza hisia na mawazo kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu, kupewa ukomo mfupi wa kumaliza kazi fulani, na hata ongezeko la mahitaji yote haya yanaweza kukuacha na wasiwasi. Hofu na kukumbwa na mambo mengi na pindi mawazo na huzuni vinapozidi uwezo wako wa kuhimili unapungua na huanza kukusababishia madhara ya mwili, kiakili na kutoridhika na kazi unayoifanya.

Ikiwa mawazo katika kazi zako huingilia utendaji wako wa kazi, afya, au maisha ya binafsi, ni wakati wa kuchukua hatua.

Haijalishi unafanya nini kwa ajili ya kuishi, au jinsi gani kazi yako inavyosababisha mawazo, kuna vitu vingi ambavyo unaweza kufanya ili kupunguza kiwango cha mawazo yako yote na kurejesha hisia za udhibiti wa kazi kikamilifu.

12.2 Vidokezo vya kukabiliana na mawazo.

(a) Shinda mawazo sehemu ya kazi kwa njia ya kushirikisha wenzako kwa msaada wa kimawazo.

Muda mwingine njia bora ya kupunguza mawazo ni kushirikisha mtu aliyekaribu na wewe. Tendo la kuzungumza na kupata msaada uso kwa uso inaweza kuwa njia yenye ufanisi sana ya kuepuka hisia na mawazo na kurejesha hali yako ya utulivu. Mtu mwingine hawezi kutatua matatizo yako; anahitaji tu kuwa msikilizaji mzuri.

(b) Rudi kwa wafanyakazi wenzako kwa msaada. Kuwa na mfumo mzuri wa msaada katika kazi inaweza kusaidia kukuzuia athari mbaya za kimawazo katika kazi yako.

Kumbuka tu kuwasikiliza na kutoa msaada wakati wanahitaji msaada pia. Ikiwa huna rafiki wa karibu kwenye kazi, unaweza kuchukua hatua za kuwa mchangamfu zaidi kwa kila mfanyakazi mwenzako. Unapopumzika, kwa mfano, badala ya kuelekeza mawazo katika simu yako, jaribu kushirikiana na wenzako.

(c) Tegemea marafiki na familia yako. Pamoja na kuongeza mahusiano ya kijamii na watu wa kazini. kuwa na mtandao imara wa marafiki na familia ni muhimu sana kudhibiti mawazo katika maeneo yote ya maisha yako.

Kwa upande wa mwingine namna unavyokuwa mpweke au mwenye kujitenga ndivyo unapozidisha kuwa na wasiwasi na udhoofu kuendelea kuwa na mawazo.

(d) Jenga urafiki mpya wenye kuridhisha. Ikiwa hujisikii kuwa na mtu yeyote wa kumfuata au kuwa nae karibu kazini

Hujachelewa sana kujenga urafiki wapya. kutana na watu wapya wenye fikra sawa na wewe kuwa nao pamoja ,toa muda wako kuwa nao karibu , Pamoja na kuwa na njia nzuri ya kupanua mtandao wako wa kijamii, kuwa mwepesi kusaidia wengine hasa wale ambao ni wenyekufurahishwa na wenyekutoa shukrani ,katika hali ya kusaidia na kutoa msaada inaweza kusaidia kupunguza mawazo.

(e) Saidia afya yako mazoezi na lishe.

Unapofanya jikita sana katika kazi, ni rahisi kupuuza afya yako ya kimwili. Lakini wakati unasaidia afya yako na lishe bora na mazoezi, unapata nguvu zaidi ya kukabiliana na mawazo. Kujijali mwenyewe haihitaji kubadilisha mfumo mzima wa maisha yako, hata mambo madogo madogo yanaweza kuinua furaha na hali yako, huongeza nguvu zako, na kukufanya uhisi kama unarudi katika hali yako ya kawaida.

(f) Tenga muda wa zoezi ya viungo mara kwa mara.

Mazoezi ya kutosha ya viungo yanayofanya mapigo ya mayo kuwa imara na kutokwa jasho-ni njia nzuri sana ya kuinua furaha yako na utulivu wa kiakili, huongeza nguvu, kuimarisha umakini wa hali ya juu, hufanya kuwa imara kiakili na kimwili.

Pia kutembea, kukimbia, kucheza, kupiga ngoma ni muhimu sana sababu hulainisha mfumo wa neva.

Ili kuwa na faraja ya kimawazo, jaribu kupata angalau dakika 30 za kupumzika wakati ukiendelea na shughuli zako za siku.

Ikiwezekana kabisa weka katika ratiba yako ya kazi muda mfupi wa kupumzika kama vipindi vitatu vya kupumzika wakati ukifanya shughuli zako za siku.Na pindi mawazo yakiendelea zaidi na kuathiri utendaji wako wa kazi, Jaribu kupumzika haraka, na tembea jinyooshe na toka sehemu yenye mawazo, toka nje ya sehemu ya kazi tembea tembea kama inawezekana kitendo cha kutembea tembea kutoka sehemu moja na nyingine hufanya upate nguvu mpya na urejee katika hali yako.

Namna unavyo chagua chakula chako inaweza kuwa na athari kubwa sana utakavyojihisi wakati wa uwapo kazini kula kidogo ila chakula chenye afya kwa mfano, inaweza kukusaidia mwili wako kudumisha kiwango cha chini cha sukari katika damu hukufanya kuwa na nguvu na kuwa na umakini na hukuepusha na hisia zisizo za lazima,

Kiwango cha chini cha sukari katika damu, kwa upande mwingine, kinaweza kukufanya uhisi wasiwasi na hasira, wakati kula sana kunaweza kukufanya uwe dhaifu, dhoofu na mwenye uchovu na uvivu.

(g) Kula kiafya.

Kupunguza sukari na kiwango cha wanga mara nyingi mtu akiwa na mawazo unakuta anapenda au kuomba vyakula viyamu vyenye kiwango cha sukari kama, bidhaa za kuokwa, au vyakula virahisi tuu kama tambi na chipsi ila vyakula hivi hupelekea kudhoofisha mwili, kuongezeka kwa hisia na kuishiwa nguvu na hufanya hali ya kuwa na huzuni na mawazo kuzidi kuliko kupungua.

- Kupunguza ulaji wa vyakula ambavyo vinaweza kuathiri hali yako, kama vile kahawa, vyakula vya mafuta, na vyakula vilivyo na viwango vya juu vya kemikali au homoni.
- Epuka nikotini.
- Kuvuta sigara unapohisi kuwa mwenye mawazo kunaweza kukufanya kuonekana mtulivu lakini nikotini ina nguvu ya msisimko hupelekea uwoga na hofu kwa kiwango cha juu na sio cha chini.
- Kunywa pombe kwa kiasi.
- Pombe inaweza kuonekana kupunguza wasiwasi na hofu kwa muda mfupi, lakini matumizi makubwa ya pombe yanaweza kusababisha wasiwasi na hofu kwa kiwango kikubwa na huathiri hali yako uliyo nayo.

h) Usiruke muda wa kulala.

Unaweza kujisikia kama huna muda wa kupata usingizi usiku mzima, lakini kulala muda mchache kuliko kawaida kunaathiri majukumu yako ya siku ubunifu, uwezo wa kutatua matatizo na uwezo wa umakini utakavyo pumzika muda wa kutosha, ndivyo utakavyoweza kuwa makini na kufanya majukumu yako vyema na vizuri na kuweza kukabiliana na changamoto za sehemu ya kazi.

Boresha ubora wa usingizi wako kwa kufanya mabadiliko ya kiafya katika majukumu yako ya mchana na usiku. Kwa mfano, lala usiku na uamke kwa wakati mmoja kila siku katika maisha yako hata wakati wa mwisho mwa wiki kuwa makini juu ya unacho kula ns kunywa kila siku, na ufanye marekebisho kwenye mazingira yako ya kupumzikia, Lengo ni la masaa 8 ya kupumzika usiku - kiasi cha usingizi ambacho wazima wanakihitaji ili kufanya kazi kwa bora zaidi.

- Zima TV, simu yako au kompyuta yako saa moja kabla ya kulala. Kwa sababu nuru inayotokana na TV, simu ya mkononi, na kompyuta zinazuia uzalishaji wa melatonin katika muili wako hivyo huweza kuharibu kabisa usingizi wako.
- Epuka shughuli chochezi na zenye hali ya kuwazisha kabla ya kulala usiku, kama vile kufanya kazi ambazo zingefanywa mapema,

  Badala yake, jikite katika mambo ya utulivu na yasio chosha, kama vile kusoma na kusikiliza musiki, huku mwanga ukiwa wa chini.

(i) Kipaumbele na kuandaa.

Pindi mawazo ya kazi na mahali pa kazi yanakuandama kuna hatua za vitendo za kuchukua to kudhibiti hali.

- Unda ratiba yenye usawa kuwa kila kazi au majukumu ni ya msingi hakuna lisilo la msingi, Jaribu kupata usawa kati ya kazi na maisha ya familia, shughuli za kijamii na shughuli za faragha, majukumu ya kila siku na Muda wakati wa kupumzika.
- Ondoka mapema asubuhi. Hata dakika 10-15 inaweza kuleta tofauti katika siku yako nzima, aidha ufanye kazi kwa harakaharaka au ufanye kazi kwa utulivu, Ikiwa kila siku unachelewa, tega muda wako au saa ili kujipa muda wa ziada kwa lengo la kupunguza haraka haraka na mawazo katika kufanya majukumu yako.
- Panga mapumziko ya kila mara. Hakikisha kuchukua mapumziko mafupi wakati wote wa majukumu yako ukiwa kazini mfano. kutembea, kuzungumza kwa uso wa upole, au ufanyie mbinu ya kufurahi. Pia jaribu kuondoka ofisini na utoke kwenda kula nje. Itasaidia kupumzika na kurejesha nguvu na uimara zaidi.
- Kuanzisha mipaka mizuri. Wengi wetu hawaweki mipaka na matokeo yake masaa yote 24 kwa siku unakuta anaendelea kufanya kazi kupitia simu yake, kupata jumbe fupi za kikazi hata akiwa nyumbani, Lakini ni muhimu kudumisha wakati usiofanya kazi au kufikiri juu ya kazi. Hii ina maanisha kuwa usiangalie barua pepe au kupokea simu za kiofisi ukiwa nyumbani jioni, au siku za mwisho wa wiki.
- Usijitoe zaidi. Epuka kupanga ratiba zinazojirudia rudia. Ikiwa umepata majukumu mazito ni vyema kutofautisha “kupaswa” na “lazima” achana na majukumu ambayo sio ya lazima katika orodha na uyaondoe kabisa.

(j) Vidokezo vya usimamizi wa kazi kwa kupunguza mawazo katika kazi.

- Weka Kipaumbele katika shughuli zako, Fanya kwanza kazi za kipaumbele cha juu, Ikiwa una kazi ambayo ni ngumu au sio nzuri ifanye mapema zaidi, na kazi zote zitakazo baki kwako zitakuwa nyepesi.

- Gawa miradi au majukumu yako katika hatua ndogo. Ikiwa mradi au kazi kubwa inaonekana kukuchosha. Fanya kila uliwezalo kwa hatua badala ya kufanya yote kwa pamoja.
- Gawa majukumu kwa wengine. Hupaswi kufanya kila kitu wewe mwenyewe. Epuka kutamani kufanya kila jambo kwa namna hiyo utachana na mawazo yasio ya msingi katika mchakato.
- Kuwa tayari kujiweka kawaida. Wakati mwingine, ikiwa wote mnaweza kujishusha kidogo muwapo kazini wote mtaweza kupata furaha na hii itapunguza kiwango vya mawazo kwa kila mtu wenu.

(k) Achana na tabia mbaya ambazo zinachangia mawazo mahali pa kazi.

Wengi wetu hufanya kazi kuwa mbaya zaidi kutokana na mawazo na tabia mbaya.

Ikiwa unaweza kukabiliana na tabia hizi binafsi na kuzishinda, unaweza kuta muajiri anakusababishia mawazo au shida ambazo unaweza kuzidhitbiti kwa urahisi sana.

- Pinga ukamilifu. Unapojiwekea malengo yasiyo ya kweli, unajisababishia kushindwa lenga kufanya vizuri zaidi. Hakuna mtu anayeweza kuomba zaidi ya kufanya vizuri zaida
- Ondoa mawazo yako hasi. Ikiwa utajikita kuwaza kushindwa katika kila jambo na mwingiliano, utajikuta mwenyewe unaishiwa nguvu na hamasa. Jaribu kufikiri chanya kuhusu kazi yako, jaribu kuepuka wafanyakazi wenza wasio na mawazo chanya jiweke nyuma ya majukumu madogo madogo hata kama hakuna mtu mwingine anayefanya.
- Usijaribu kudhibiti tabia isio dhibitika.

  Vitu vingi kazini hatuwezi kuvidhibiti ni zaidi ya uwezo wetu hasa tabia za watu wengine, tunashindwa kudhibiti vyema badala yake tunawasababishia mawazo, fikiria mambo ambayo unaweza kudhibiti kama vile unavyochagua kushughulikia matatizo.
- kuwa na hali ucheshi na furaha katika hali hiyo. Wakati unatumiwa ipasavyo katika majukumu yako, ucheshi ni njia nzuri ya kupunguza matatizo na mawazo katika sehemu ya kazi. Wakati wewe unapoanza kuchukua mambo kwa uzito sana, tafuta njia ya kupunguza uzito huo kwa kushirikiana na rafiki zako kicheka na kutaniana pamoja.
- panga na weka matendo na vitu vyako sawa. Ikiwa meza yako au nafasi yako ya kazi ni chafu, safisha na ondoa uchafu wote uliopo mezani kwako kwa kazi; kujua tu namna gani kitu kinaweza kuokoa muda na kupunguza mawazo.
- Kuwa zaidi ya makini na imara katika kazi yako na majukumu yako ya kiofisi na mahali pa kazi. Unapojisikia vibaya wenye mawazo wasio na uwezo wa kudhibiti mawazo hayo kwa kiwango kikubwa

Hapa kuna baadhi ya mambo unayoweza kuyafanya ili upate upya hisia ya udhibiti juu ya kazi yako na majukumu yako.

- Ongea na mwajiri wako kuhusu wasiwasi na shida za sehemu ya kazi Wafanyakazi wenye afya na wenye furaha wanaozalisha zaidi, hivyo mwajiri wako ana wajibu wa kudhibiti matatizo yaliyopo sehemu ya kazi wakati wote inapowezekana. Pia vyema kuorodhesha malalamiko na matatizo yaliyopo sehemu ya kazi ili mwajiri wako ajue kuhusu hali maalum ambazo zinaathiri utendaji wako wa kazi.
- Fahamu maelezo na ufafanuzi wa kazi yako. Muombe msimamizi wako kwa maelezo mapya ya kazi na majukumu yako. Pia unaweza kutenga na kuchagua kufanya kazi ambazo sio sehemu ya maelekezo au ufafanuzi wako wa kazi, ili kupata kungwa mkono na kuonekana muwajibikaji kwa kuonesha kuwa ukifanya majukumu zaidi hata ya yale yalio katika ufafunuzi na muongozo wa kazi zako.
- Omba uhamisho. Ikiwa eneo lako la kazi ni kubwa sana, unaweza kuepuka mazingira mabaya kwa kuhamishwa kwenye idara nyingine.
- Omba kazi mpya. Ikiwa umekuwa ukifanya kazi hiyo hiyo kwa muda mrefu, omba kujaribu kitu kipya: katika kiwango cha daraja tofauti, eneo la kazi tofauti, na utendaji tofauti.
- Chukua muda wa mapumziko nenda likizo, tumia siku zako za ugonjwa, uomba kuondoka kwa muda mfupi. Tumia muda huo kurejesha nguvu zako na kuchukua mtazamo mpya.

(i) Jinsi waajiri wanavyoweza kupunguza mawazo na matatizo Kazini

- Shauriana na waajiriwa wako. Zungumza nao juu ya mambo maalum ambayo hufanya kazi zao kuwa ngumu. Vitu vingine, kama vile ubovu wa vifaa, uhaba wa wafanyakazi, au ukosefu wa wawasimamizi. Kubadilishana mawazo na kuhabarishana changamoto kazini kunaweza kupunguza wasiwasi, hofu na mawazo katika kazi na hatima yao.
- Wasiliana na wafanyakazi wako mmoja mmoja wasikilize kwa makini uso kwa uso utafanya wafanyakazi kujisikia kusilizwa na kuelewaka na kusaidia kupunguza matatizo, mawazo yao na yako-hata kama huwezi kubadilisha hali iliyopo.
- Shughulikia migogoro ya mahali pa kazi kwa njia nzuri. Kuheshimukila mfanyakazi; kuanzisha sera ya kutovumilia unyanyasaji.
- Wawezeshe wafanyakazi fursa kushiriki katika maamuzi yanayoathiri kazi zao. Wape wafanyakazi fursa za mawazo yao katika mchakato wa kuandaa sheria na taratibu za kazi kwa mfano. Ikiwa wamehusika katika mchakato huo, watakuwa thabiti na hamasa kubwa.
- Epuka kuweka muda usiofaa kwa wajiri au wafanyakazi juu ya muda wa mwisho (deadlines) kuwasilisha kazi, hakikisha majukumu unayoyatoa yanaendana na uwezo wa wafanyakazi na vitendea kazi na rasilimali.
- Eleza matarajio yako fafanua waziwazi wajibu, majukumu, na malengo ya wafanyakazi. Tengeneza vitendo vya usimamizi vizuri na thabiti vyenye kuenda sambamba na maadili ya shirika.
- Kutoa tuzo na zawadi kama motisha. Sifu utendaji mzuri wa kazi kwa shirika kwa ujumla. Weka ratiba ya kipindi kigumu chenye majukumu mengi ikifuatiwa na kipindi chenye majukumu machache yasio bana sana. Toa nafasi kwa wafanyakazi kukutana na kushirikiana kwa kukutanishwa kwa masuala ya kijamii.

Marejeo na viunganisho vya msingi.

1. Kitabu cha ulinzi wa watetezi wa haki za Binadamu 2005, kimeandaliwa na watetezi wa haki za Binadamu
2. Ripoti ya hali ya watetezi wa haki za Binadamu nchini Tanzania, 2013,2014,2015,2016, na 2017 imeandaliwa na Mtandao wa watetezi wa haki za Binadamu.
3. Muongozo wa usalama kwa watetezi wa haki za Binadamu barani Afrika, 2017 imeandaliwa na watetezi wa haki za Binadamu.

Viunganisho muhimu.

http://locdoc.net/security-and-locksmithing-blog/8-simple-steps-youcan-take-to-improve-your-office-security-today/

https://www.helpguide.org/articles/stress/stress-in-the-workplace. htm

https://www.apa.org/helpcenter/work-stress.aspx

https://security.berkeley.edu/resources/best-practices-how-toarticles/top-10-secure-computing-tips

https://www.zdnet.com/article/simple-security-step-by-step-guide/

https://www.theguardian.com/technology/2013/sep/16/10-wayskeep-personal-data-safe

https://www.afgonline.com.au/learn/home/top-10-tips-to-improveyour-home-security/

Orodha ya Sheria

Sheria ya Makosa ya Mtandao 2015

Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, 2016

Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, 2017

Kanuni za Maudhui ya mtandaoni, 2018

Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi 1969.

Sheria ya Tawala wa Mikoa, 1997

TANZANIA HUMAN RIGHT DEFENDERS COALITION (THRDC)
Eyasi Road, Near Hekima Garden, P.o.box 105926, Dar Es Salaam, Tanzania
+255 769 64220
thrddefenders@gmail.com
www.facebook.com/TanzaniaHumanRightsDefendersCoalition
www.thrd.or.tz